
# MWENGE WA UHURU NA UKOMBOZI WA FIKRA



ISBN 978-9976-5-7131-8

9 789976 571318 >

## MWANAWETU MMUNI

**Hakimiliki zote zimehifadhiwa © Mwanawetu Mmuni**

Kitabu hiki kimeandikwa na:-
Mwanawetu Mmuni
P. O BOX 90,
**Mtwara - Tanzania**
Email: Mwanammuni@gmail.com
Simu: +255 737966996

Kimechapishwa na;
Lulu Selfpublishers
Chapa ya kwanza eBook © 2020

**© 2021**

ISBN: 9 789976 571318 >

Haki zote zimehifadhiwa, hairuhusiwi kuiga, kunakili, kufasiri, kuchapa, au kutoa kitabu hiki kwa njia yeyote ile bila idhini ya Mwandishi

# YALIYOMO

YALIYOMO .... 3
SHUKRANI .... 4
UTANGULIZI .... 5
HISTORIA YA MWENGE .... 7
DHANA YA MWENGE WA UHURU .... 10
MWENGE WA UHURU ULIWASHWA LINI ZANZIBAR? .... 16
UHUSIANO WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU NA MAENDELEO YA KIUCHUMI TANZANIA .... 21
ELIMU .... 23
HISTORIA YA MWENGE NA UCHAWI .... 33
MKESHA WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU .... 39
ITIKADI ZA KISIASA NA VYAMA VYA SIASA .... 46
VYAMA VYA SIASA .... 51
BAJETI YA MBIO ZA MWENGE .... 56
HISTORIA YA UKOMBOZI WA TANGANYIKA .... 68

# SHUKRANI

Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uhai. Pia shukrani zangu ziifikie familia yangu kwa uvumilivu wao, Mama yangu aliyejitoa kadri ya uwezo wake kuhakikisha ninakua vizuri na kupata elimu, Dada na Kaka zangu kwa kuniunga mkono.

Shukrani zangu za dhati zifike kwa; Dkt. Harrison Mwakyembe (PhD) aliyekuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, na Mhandisi Stella Martin Manyanya (Mbunge) aliyekuwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara kwa kutambua kazi zangu. Ninakushukuru Mhe Dunstan Kyobya (DC-Mtwara), Madam Erica Yegella (DED-Mtwara DC) pamoja na viongozi wote wa chama na serikali wa mikoa ya Lindi na Mtwara. Ninawashukuru sana Wahadhiri (MUCE) waliosimamia Elimu yangu, Bw. Chris Park na familia yake (UK) kwa kugundua kipaji changu cha uandishi, Dkt. Alawi Mikidadi (PhD) kwa kutumia muda wako kusoma mswada wa kitabu hiki na kusanifu, Dkt. Makulilo E (PhD) na Prof. Mbele (U.S.A) kwa ushauri wa uandishi na uchapishaji vitabu mtandaoni, Bw. Richard Uswege-mchoraji,  Bw. Thomas Safari (DAS-Lindi), Bw. Masuha (Afisa Habari Mtwara), Clouds Media, Hopaje TV, Safari Radio,  Bw. Jerry na Uongozi wa Pride Radio, Bw. Elibariki Mafole (Afisa Habari Lindi), Bw. Abdulaaziz na Bw. Beda (Mwananchi).

Katika kukamilisha kazi hii ya uandishi nimeweza kupata ushirikiano toka kwa rafiki zangu na Wafanyakazi wenzangu. Hivyo ninawashukuru kwa subra zao, Pia ninawashukuru washirika wangu; Wachapishaji, Wasambazaji na Wasomaji wa nakala za maandiko yangu. Asanteni sana!

# UTANGULIZI

Mwenge wa Uhuru wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania una thamani kubwa kwa Watanzania kwa kuwa kuwashwa kwake kumebeba dhamira ya ukombozi wa nchi toka kwa wakoloni. Hii ni falsafa iliyotumika kutoa hamasa ya ukombozi wa fikra kwa Watanganyika na baadae kwa Watanzania wote kama kauli ya Baba wa taifa ilivyojieleza.

*"Sisi (Watanganyika) tunataka kuuwasha Mwenge na kuweka juu ya mlima Kilimanjaro, umulike hata nje ya mipaka yetu; ulete tumaini pale ambapo hakuna matumaini, upendo mahali palipo na chuki na heshima palipojaa dharau" (Nyerere, 1959).*

Mbio za Mwenge zinazoongozwa na vijana wakakamavu zinahimiza wananchi kutimiza wajibu wao kila mmoja kwa nafasi yake ili; hujuma, dhuluma, ubaguzi, matabaka, ufisadi, unyonyaji, rushwa, uzembe, matumizi mabaya ya ofisi, wizi, uvivu, umaskini, maradhi, matumizi ya madawa ya kulevya, njaa, na vita visiwepo katika maisha ya Watanzania. Pia zinakumbusha kudumisha uzalendo, matumizi sahihi ya sayansi na teknolojia, kusisitiza vijana kuunga mkono juhudi za serikali katika kuleta maendeleo pamoja na kulinda amani ya nchi na mipaka yake.

Uwepo wa Mwenge wa uhuru juu na kilele cha mlima Kilimanjaro, mlima mrefu Barani Afrika ni ishara ya sauti za Watanzania kuwa na nguvu katika kudai Ukombozi. Wananchi wenye fikra zinazoweza kumulika hadi nje ya

mipaka ya nchi na kung’ara kama barafu za kilele cha mlima Kilimanjaro. Watu wote wenye nia mbaya juu ya maisha na maendeleo ya Watanzania katika Tanzania huru, Mwenge wa Uhuru utawamulika na kuwachoma.

# HISTORIA YA MWENGE

Mwenge wa uhuru wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, uliwashwa na kuwekwa kwenye kilele cha mlima Kilimanjaro tarehe 09 ya mwezi Desemba, mwaka 1961. Mwanzilishi wa mwenge huu ni Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa kwanza wa Tanganyika kwa sasa Tanzania.

Miaka miwili kabla ya uhuru wa Tanganyika kutoka kwenye ukoloni wa Waingereza yaani 22 Oktoba, 1959; Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akiwa anahutubia Baraza la kutunga sheria (Legislative Council - LEGICO) kipindi hicho alikuwa Mwenyekiti wa chama cha TANU na mjumbe wa LEGICO alisema; "Sisi (Watanganyika) tunataka kuuwasha mwenge na kuweka juu ya mlima Kilimanjaro, umulike hata nje ya mipaka yetu; ulete tumaini pale ambapo hakuna matumaini, upendo mahali palipo na chuki na heshima palipojaa dharau". Mwenge ulipandishwa na kuwekwa juu ya kilele cha mlima Kilimanjaro na shujaa Luteni Kanali Alexander Nyirenda, (Michuzi, 2018). Kiongozi mwasisi wa taifa la Tanzania alisisitiza kuwa mwenge wa uhuru una umuhimu mkubwa katika kuijenga Tanganyika yenye umoja, mshikamano na upendo miongoni mwa wananchi wake na kusababisha nchi kuwa miongoni mwa nchi zile zinazosifika kwa amani na utulivu duniani kote.

Hivyo kila wakati taifa linawajibu wa kujikumbusha bila ya kuchoka kuhusu dhana na falsafa hiyo kupitia maneno

aliyoyatamka katika hotuba zake ambayo yalijaa uzalendo, busara, hekima, na upendo kwa nchi yake kabla na baada ya uhuru.

## Maana ya neno mwenge

Mwenge ni kitu kilicho na utambi ulio katika chombo kama kikombe chenye mpini ambacho huwashwa na kukimbizwa katika kusherehekea jambo fulani (TUKI, 2004). *Mwenge* unafanana na kibatari (koroboi) inayotumia mafuta ya taa. *Mwenge* ni fungu la vijiti au kipande cha kuni kinachowaka hutumiwa na wakazi wa vijijini kupata mwanga.

## Mwenge wa uhuru

Ni chombo kilichotengenezwa kwa kutumia madini ya chuma, shaba, bati na mti aina ya mpingo au mninga. Kipande cha mti ni sehemu ya mshikio. Tenki la kuhifadhia mafuta ya mwenge hutengenezwa kwa chuma na huunganisha ndimi za utambi kwa ajili ya kuwaka. Mwenge wa uhuru wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania una uzito wa ratili kumi kabla ya kuwekwa mafuta. Mwenge huu unatengenezwa na kampuni moja maarufu nchini Tanzania.

## Ukombozi ni nini?

TUKI, (2004), Ukombozi ni matendo au vita vya kuokoa watu kutoka kwenye hali mbaya yenye mateso au hali ya unyonge.

## Uhusiano wa mwenge wa uhuru na ukombozi wa Tanganyika

Mwenge wa uhuru haukuwashwa na kukimbizwa nchi mzima kwa lengo la kuleta mwanga au nuru kama myenge mingine ifanyavyo. Bali uliwashwa kwa lengo la; kuleta tumaini pale ambapo hakuna matumaini, upendo mahali palipo na chuki na heshima palipojaa dharau. Maneno haya yakifalsafa na kiharakati yalitamkwa na Mwenyekiti wa Chama cha TANU kwa lengo la kuwaongezea wananchi hamasa na tamaa ya kujikomboa kutoka kwenye utawala wa kikoloni ulioongozwa na Gavana wa Uingereza Richard Turnbull akimwakilisha Malkia. Mwenge wa uhuru ulitumika kutia imani ya ukombozi wa fikra na kujitawala kwa Watanganyika.

# DHANA YA MWENGE WA UHURU

Dhana ya mwenge wa uhuru ina mitazamo minne (4) nayo ni;

1. Mtazamo wa kitamaduni
2. Mtazamo wa kisiasa
3. Mtazamo wa kiuchumi
4. Mtazamo wa kifalsafa

## 1. MTAZAMO WA KIUTAMADUNI

Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alizaliwa Butiama April 13 ya mwaka 1922. Alikuwa miongoni mwa watoto 26 wa Nyerere Burito ambaye alikuwa Chifu (Mtemi) wa kabila la Wazanaki. Ibada ya mwenge ni sehemu ya matambiko ya wenyeji wa Butiama mkoani Mara. Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliishi na mama yake Bi. Mgaya Nyang'ombe katika eneo la Mwitongo na watu wengi huita Mwenge wa Uhuru, "Mwenge wa Mwitongo." Nako mwenge huachwa unawaka hadi kuzima wenyewe unapoishiwa mafuta. Jina la Kambarage alilipata baada ya kuzaliwa siku ya mvua na kupewa jina hilo likiwa na maana ya (mzimu wa mvua). Wakati jina la Julius aliitwa baada ya kubatizwa na kuwa Mkatoliki na akajipa Jina la “Julius”.

Usiri uliopo wakati wa kuwashwa mwenge wa uhuru na kuzimwa unahusishwa na masuala ya mila. Pia unapositiriwa kwenye chumba maalum pindi unapozimika

ghafla au kubadilishwa, au kuongezwa mafuta, hali hii watu wenye mtazamo wa mambo ya asili wanatafsiri kuwa; kuna imani za kishirikina katika shughuli za mwenge huo wa uhuru.

Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliaga dunia mnamo Oktoba 14, 1999 katika hospitali ya Mtakatifu Thomas iliyopo Mjini London Uingereza. Ingawa yeye (Mwalimu Julius Kambarage Nyerere) amefariki, Watanzania wanaendelea kuamini, kuyaenzi na kuyaendeleza yale yote mema na yenye tija kwa taifa yaliyoachwa na Mwasisi, (Msekwa, 2012). Kwa kuzingatia hayo, mnamo tarehe 14 Oktoba, 2019; Rais wa awamu ya tano wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli (PhD), aliwahutubia Wananchi wa Tanzania kupitia wakazi wa mkoa wa Lindi katika sherehe za kuzima Mwenge (kilele cha mbio za mwenge) huo pamoja na maadhimisho ya kumbukizi ya miaka 20 tangu kufariki kwa mwasisi wa taifa (Baba wa taifa), kiongozi wa ukombozi. Rais alitumia fursa hiyo kuwaongezea imani ya uzalendo wananchi juu ya mustakabali wa taifa pamoja maendeleo yake ya kiuchumi.

## 2. MTAZAMO WA KISIASA

Wapo wanaosema, "mwenge wa uhuru uliwashwa ili kutoa hamasa ya ukombozi kwa wapigania Uhuru." Mwenyekiti wa chama cha TANU, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alitamka "Sisi tunataka kuuwasha mwenge na kuweka juu ya mlima Kilimanjaro, umulike hata nje ya

mipaka yetu; ulete tumaini pale ambapo hakuna matumaini, upendo mahali palipo na chuki na heshima palipojaa dharau."

*Mwenge wa uhuru umeleta ukombozi wa fikra kwa namna mbili. Nazo ni; kauli, na alama.*

## A) Kauli

Kauli ya kimkakati aliyoirudia kuitamka tena baada ya miaka miwili; Ni miongoni mwa kauli iliyotumika kuleta hamasa kwa Wanachama wa chama cha TANU pamoja na wananchi kuhusu ukombozi wa nchi yao ambayo kwa wakati huo ilitawaliwa na mkoloni. Hivyo Mwenge wa Uhuru na dhamira ya kuanzishwa kwake ni kujenga hamasa ya kutamani kujikomboa kutoka kwenye dhuluma, dharau, kutawaliwa, kunyanyaswa, kubaguliwa, chuki, kukandamizwa kutoka kwenye serikali ya kibepari wenye kuongozwa kwa matabaka. Wakati huo ilikuwa ni tabaka la watawala na watawaliwa yaani Watanganyika (wazawa) na wakoloni pamoja na wafuasi wao wachache.

## B) Alama

Mwenge wa uhuru ni chombo kilichotumika kuwekea ahadi ya kauli iliyotamkwa kuhusu ukombozi. Katika jamii au familia tumekuwa tukitumia vifaa au vyombo au vitu mbalimbali kuwekea ahadi. Vitu hivyo, vyaweza kuwa duni sana lakini kutokana na ahadi iliyowekwa pindi alama hiyo inawekwa au kitu kutumika; hufanya kitu hicho pia kuwa

muhimu na cha thamani zaidi. Kwa mfano pete kwenye ndoa au cheti kwenye taaluma.

Pia mwenge wa uhuru unawakumbusha wanasiasa kutimiza ahadi wanazozitoa kwa wananchi kwa maslahi ya taifa. Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliahidi kuwasha Mwenge na kuweka juu ya mlima Kilimanjaro mwaka 1959 alipolihutubia Baraza la kutunga sheria na baada ya miaka miwili tu yaani tarehe 09 Desemba, 1961; Mwenge wa Uhuru uliwashwa na kuwekwa juu ya kilele cha mlima Kilimanjaro.

## Baraza la Kutunga Sheria

Historia ya baraza la kutunga sheria la Tanganyika; lilianzishwa tarehe 07 ya mwezi Desemba mwaka 1926 na kuzinduliwa Jijini Dar-es-salaam chini ya Mwenyekiti wake aliyekuwa Gavana wa Tanganyika, Sir Donald Cameron. Jukumu la Baraza ni kufanyiakazi mapokeo ya sheria kutoka bunge la Uingereza. Wajumbe wa baraza hili waliteuliwa na Mwenyekiti wake ambaye ni Gavana. Novemba 1, mwaka 1953; Spika wa kwanza aliteuliwa na kuchukua nafasi ya Gavana, hivyo Spika alishika wadhifa wa kuwa kiongozi na kuwa Mzungumzaji mkuu katika baraza hilo (Msekwa, 2012).

Mwaka 1958, kulitokea uchaguzi wa kwanza ulioruhusiwa katika kipindi cha ukoloni. Uchaguzi huu ulishirikisha vyama vya siasa vya Watanganyika ndipo vyama kama vile United Tanganyika Party (UTP), All Muslim National Union of Tanganyika (AMNUT), Tanganyika National

union (TANU) na African National Congress (ANC) viliposhiriki katika kinyang'anyiro hicho cha kupata wajumbe wawakilishi katika Baraza la kutunga sheria. TANU ilishinda kwenye baadhi ya majimbo na hivyo kuwa chama cha kwanza kuwa na Wanachama katika Baraza la kutunga sheria. Uchaguzi huu uliweza kuwapata wawakilishi wachache waliochaguliwa na wananchi.

Mnamo mwaka 1960, Baraza lilibadilishwa jina na kuitwa Bunge. Kwa kuwa katiba ya Malkia wa Uingereza hupitisha sheria iliyotungwa na Baraza la kutunga sheria, baada ya Tanganyika kuwa na bunge lake Uingereza haikuwa na mamlaka ya kutunga sheria tena. Bunge liliendelea kuwa na mamlaka ya kutunga sheria kama ilivyokuwa kwa Baraza la kutunga sheria.

Hivyo kwa mujibu wa historia hii inatuonesha kwamba; Baraza lililoridhia mwenge wa uhuru kuwashwa na kuuweka juu ya kilele cha mlima Kilimanjaro lilikuwa ni Bunge tukufu la Tanganyika.

## 3. MTAZAMO WA KIUCHUMI

Baada ya kuangalia mtazamo wa kiutamaduni na kisiasa, sehemu hii inaelezezea mtazamo wa kiuchumi. Yaani Mwenge wa uhuru unatija gani kiuchumi kwa wananchi wa Tanzania.
Wapo baadhi ya watu wanaolaumu kuwa bajeti ya mbio za mwenge wa uhuru kwa mwaka ni kubwa kuliko miradi inayozinduliwa, hivyo ni hasara.

Mwenge wa uhuru unakimbizwa nchi mzima kwa siku zaidi ya 190 katika mikoa yote 31 ya Tanzania bara na Tanzania visiwani; ukipita kwenye kata / shehia, wilaya na mikoa. Hivyo basi, unaendelea kuwakumbusha wananchi wajibu wa kufanyakazi kwa bidii ili kuleta maendeleo huku ukitumika kuzindua miradi mbalimbali kila mwaka kwenye maeneo hayo. Kauli mbiu na ushindani kiwilaya na kimkoa huleta mafanikio makubwa.

Miradi mipya inazinduliwa kila mwaka ikiwa imebeba ujumbe unaoendana na kauli mbiu ya mwaka huo. Mfano wa kauli-mbiu za mbio za mwenge ni; "shiriki kukuza uchumi wa viwanda kwa maendeleo ya nchi," na “Walanguzi - mwenge choma, wezi - mwenge choma, wanaoiba fedha za umma - mwenge choma, wavivu-mwenge choma.” Kauli mbiu hizi zilitungiwa nyimbo zilizotumika kusherehesha kipindi cha mbio za mwenge.

Kwa hekima za viongozi wa mbio za Mwenge, miradi inayozinduliwa ni ile iliyokamilika na kukidhi thamani halisi ya fedha 'value for money' zilizotumika kujenga au kukamilisha mradi huo. Miradi yenye harufu ya rushwa, isiyokamilika, yenye ubadhirifu wa fedha haizinduliwi na mwenge wa Uhuru. Badala yake viongozi na wote walioshiriki kusimamia mradi huo wanawajibishwa kwa manufaa ya umma. Mfano mwaka 2018, Kiongozi Mkuu wa mbio za mwenge Mhe. Charles Kabeho; alikataa kuzindua miradi mingi baada ya kuona kuna dalili ya rushwa na matumizi mabaya ya fedha. Miradi iliyokataliwa

ilikabidhiwa mikononi mwa TAKUKURU ili ishughulikiwe inavyostahili na wahusika wachukuliwe hatua za kisheria.

Mbio za mwenge wa uhuru zilianza rasmi baada ya uhuru kama ilivyoelezwa katika “Government portal” kuwa; "After independence the government decided to launch Uhuru Torch Races for mobilizing the people to participate in various political, social and economic endeavors." “Since 2000, The races starts from one chosen region and end on 14th October the day we commemorate the death of the father of the nation Mwalimu Julius Kambarage Nyerere” (Government, 2015).

## MWENGE WA UHURU ULIWASHWA LINI ZANZIBAR?

Zanzibar na Tanganyika ziliungana Aprili 26, 1964 na kuwa nchi moja iliyopewa jina la “Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar” na baadae kuitwa “Jamhuri ya Muungano wa Tanzania” mnamo tarehe 28 Oktoba, 1964 kupitia sheria ya Jamhuri ya Muungano namba 61 ya mwaka 1964. Makala ya Muungano kwenye Msekwa, (2013), imeeleza tamko hilo kuwa; “The people’s Republic of Zanzibar and the Republic of Tanganyika shall, upon union Day and forever after be united into one Sovereign Republic by the name of the United Republic of Tanganyika and Zanzibar.” Kwa hiyo, mwenge wa uhuru uliwashwa visiwani Zanzibar yaani Unguja na Pemba baada ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964.

# 4. MTAZAMO WA KIFALSAFA

Kupitia hotuba za Mwasisi wa mwenge huo wa uhuru yaani Baba wa taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliweza kutafsiri falsafa iliyopo katika maneno aliyoyatamka siku ya kupandishwa kwa mwenge huo juu ya kilele cha mlima Kilimanjaro. "Tunauwasha mwenge na kuuweka juu ya mlima Kilimanjaro, umulike hata nje ya mipaka yetu ili ulete tumaini ambapo hakuna matumaini, upendo mahali palipo na chuki na heshima palipojaa dharau."

## Ukombozi wa fikra katika mtazamo wa kifalsafa

1. "**Sisi (Watanganyika)** tunataka kuuwasha Mwenge." Inaonesha kuwashwa kwa mwenge wa uhuru sio jambo la mtu mmoja, au kikundi cha watu, au itikadi ya chama bali ni dhamira yenye umoja na mshikamano baina ya wananchi bila kujali itikadi, cheo wala nyadhifa za watu. Viongozi wa Tanganyika na wananchi wote kwa pamoja walikuwa na kauli moja. Hivyo, mwenge wa uhuru kupandishwa mlima Kilimanjaro ni kutokana na kauli ya makubaliano ya wananchi wa taifa zima. Kauli hii ilitamkwa 22 Oktoba, 1959 na utekelezaji wake ulifanyika 09 Desemba, 1961.

**2. "Kuwasha mwenge**" ni alama ya kujaza ujasiri wa kifikra katika kuamua kufanya jambo lao muhimu ambalo lilikuwa kujikomboa kutoka katika minyororo ya wakoloni. Mwenge ni miongoni mwa vyombo vilivyotumika kuwapa wananchi hamasa ya ujasiri wa kudai haki.

**3. "Mlima Kilimanjaro**" ni mlima mrefu Barani Afrika. Kitendo cha kuweka Mwenge wa Uhuru unaowaka juu ya kilele cha mlima huu mrefu; ni sawa na kupaza sauti. Baada ya tukio hilo kuliipa nguvu sauti ya Watanganyika ya kudai haki na ukombozi wa nchi yao kutoka kwa wakoloni (uhuru). Kuthibitisha hili, wakoloni walikubali kutoa uhuru mwaka 1961 lakini bado nchi ilikuwa sio Jamhuri. Baba wa taifa alisalia kuwa Waziri Mkuu hadi ilipofika 1962 mwaka mmoja baada ya mwenge wa uhuru kuwashwa na kupandishwa juu ya kilele cha mlima Kilimanjaro. Ndipo mabadiliko yalipotokea na Tanganyika ikawa Jamhuri na kujitwalia Rais wa kwanza ambaye ni Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

**4. "Umulike hata nje ya mipaka yetu"** Ukombozi haukubakia kwa Watanganyika pekee bali ulifika nje ya mipaka ya Tanganyika hadi ukafika kwenye nchi nyingine za Afrika. Hivyo, sauti ya Watanganyika iliyowekwa juu ya kilele cha mlima Kilimanjaro iliweza kusikika na kuwa na nguvu ya kutoa hamasa za ukombozi kwa wapigania uhuru kutoka kwenye mataifa jirani ya Afrika ya Kusini na Mashariki. Sio sauti pekee bali hata ardhi ya Tanganyika na Watanyanyika wenyewe walijitoa mhanga kuwahifadhi Waafrika wenzao kwa kuwapa makazi. Eneo kama Kongwa mkoani Dodoma lilitumika kuwahifadhi viongozi wapigania uhuru toka nchi mbalimbali mfano Msumbiji - Hayati Samora Machel, Sam Nujoma wa Namibia, Hifikepunye Pohamba wa Namibia na wengine wengi. Maeneo mengine yaliyotumiwa na wakimbizi-wapigania uhuru toka kwa wakoloni ni Mazimbu, Dakawa Mkoani

Morogoro hivyo yalikaliwa na African National Congress kuanzia mwaka 1982 hadi 1992.

(Nyerere, 1967), "Tumezielekeza fikra hizi waziwazi katika kanuni za taifa letu katika Azimio la Arusha na katika matamko mengine yaliyotangulia, tumetaja misingi na siasa yetu na hatima ni umoja wa Afrika mzima. Na kwamba tutafanya juhudi kufikia lengo hilo, lakini kwa sasa tutalinda heshima na Uhuru wa Jamhuri ya Muungano." Mwalimu Nyerere pia alieleza kwenye kitabu chake, ninanukuu; "Hata hivyo ni dhahiri kwamba, kama tunataka kupiga hatua kuelekea lengo hilo, sisi watu wa Tanzania hatuna budi tukubali hali yetu ya ndani ya nchi na hata nje, halafu tufanye bidii kuibadilisha hali hiyo ilingane na shahada yetu."

5. **Kuleta heshima palipojaa dharau.**

*Dharau* ni tabia ya kukosa kuthamini na kuheshimu mtu au watu, (TUKI, 2004). *Dharau* ni tabia ya mtu ya kupuuza mambo na kutofuata kanuni au taratibu zilizowekwa. **Heshima** ni thamani ya ubinadamu. Au, *heshima* ni kitu anachopewa mtu kama alama ya kuthaminiwa kwake.
Dharau haiwezi kutoweka bila elimu. Iwe kwa kumuelimisha mtu mwenye dharau juu ya athari za kufanya dharau na/au aliyedharauliwa anatakiwa kuelimishwa ili ajikomboe kutoka kwenye minyororo ya dharau na udhalilishwaji.

**Heshima inapatikanaje?**

Katika falsafa ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika kulijenga taifa alitanguliza shahada ya kutoa elimu.

Je, elimu iliyokusudiwa kutolewa ilitosha kumtoa Mtanzania katika minyororo ya dharau?

## UHUSIANO WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU NA MAENDELEO YA KIUCHUMI TANZANIA

Kuna mambo mengi yanayohusiana kati ya mbio za mwenge na maendeleo ya uchumi wa nchi, nitayataja machache:

1. Mwenge wa uhuru kutumika kama sauti ya wananchi katika kuhoji utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

2. Mikutano ya mbio za mwenge wa uhuru inatumika kukusanya kero za wananchi hasa vijijini ambako viongozi wengi hushindwa kutembelea na kuandaa mikakati ya kutatua kero hizo. Taarifa zinamfikia kiongozi wa mbio za mwenge kwa njia ya kusikiliza risala mbalimbali, nyimbo, hotuba za viongozi na mazungumzo ya ana kwa ana wanapopita kwenye maeneo yao.

3. Kukumbusha uwajibikaji wa viongozi wa serikali katika kutekeleza majukumu yao. Miradi inayotarajiwa kuzinduliwa na kiongozi wa mbio za Mwenge, lazima ikaguliwe kwanza na viongozi wa serikali ngazi ya wilaya na katika ngazi ya mkoa. Ili kuona kama inakidhi thamani halisi ya fedha kwa miradi inayotarajiwa kuzinduliwa ili kuepuka upotoshwaji wa dhamira ya mbio za mwenge wa uhuru. Kuziba mwanya wa rushwa na kuzindua miradi yenye maendeleo endelevu badala ya miradi

ya maonesho na baada ya mwenge wa uhuru kupita, miradi kukosa uzalishaji au huduma.
4. Kuhamasisha vijana kujitolea kushiriki katika shughuli za kiuchumi katika kujiendeleza na maendeleo ya nchi kwa ujumla.
5. Kujenga uzalendo katika kushiriki ujenzi wa taifa kwa kujitoa kwa juhudi na maarifa.
6. Kukumbusha kulinda uhuru, umoja, amani, na utulivu. Vikikosekana, uchumi wa nchi unadumaa.
7. Kubuni miradi itakayozinduliwa na mbio za mwenge wa uhuru hivyo kurahisisha huduma kwa wananchi.

Mwenge unatumika kuhamasisha na kutoa elimu kwa Watanzania kutoka kwenye mifumo ya kutawaliwa na kunyonywa kisha wajikite katika kuzalisha mali na kuwa Jamii inayojitegemea.

Kwa mintarafu ya mambo tajwa hapo juu serikali ya awamu ya tano ya Rais Dkt. John Magufuli (PhD), imedhamiria kukuza uchumi wa viwanda kwa kufufua viwanda vilivyopo na kuanzishwa viwanda vidogo na vikubwa.

# ELIMU

Baada ya Tanganyika kupata Uhuru na mwenge kuwashwa, bado Watanganyika waliishi gizani. Hivyo katika kukamilisha falsafa ya ukombozi wa Mwafrika, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliweka kipaumbele cha elimu katika kulijenga taifa la Tanganyika.

Ingawa elimu iliyokuwa inatumika bado ilikuwa na mifumo ya kibepari iliyorithiwa kutoka kwa wakoloni. Hivyo bado iliweka matabaka ya walionacho na wasionacho, watawala na watawaliwa, wamjini na wakijijini, wazalishaji na walaji. Hilo lilifafanuliwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere baada ya kueleza katika hotuba zake alizohutubia Wananchi baada ya kuwashwa mwenge wa uhuru na kuwekwa juu ya kilele cha mlima Kilimanjaro.

## Elimu kabla ya uhuru

Katika (Nyerere, 2004), ilichapishwa hotuba ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ya mwaka 1967 yenye kufafanua muundo wa elimu ya kikoloni ambayo ilikuwa ya kibaguzi na kutaja maazimio ya serikali katika kuwaondolea dharau wananchi wake. Alisema, “kwa muda mrefu sana sisi katika nchi hii tumeugua ugonjwa wa fikra za kikoloni ambazo ijapokuwa ukoloni wenyewe kweli umeondoka, lakini ugonjwa wa fikra za kikoloni bado upo. Watu hufikiri kuwa wasichana na wavulana wetu wakishapata elimu halafu wakirudi nyumbani kuwa wakulima, eti wamepoteza elimu yao. Ndiyo kusema kwamba eti ukulima hauhitaji elimu yeyote, kuwa kila mtu anaweza kulima na lisiharibike neno. Fikra za namna hii ni

mbaya katika Jamhuri ya Muungano ya 1964. Maendeleo yetu ya kila upande yanategemea zaidi wakulima kuliko raia wengine wowote. Wao ndio waliopewa madaraka ya kutumia amali yetu kubwa, yaani ardhi." Alikazia kwa kusema; "kama wakulima ni wajinga wasiotaka mabadiliko na maendeleo, basi taifa letu vile vile litakuwa taifa jinga lisilotaka maendeleo wala mabadiliko. Wakulima wasipopata ujuzi na elimu itakayowawezesha kufikiria maendeleo na maisha bora, basi majumba yale mazuri ya mijini, barabara zetu na vyote vingine ni bure."

Wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanapaswa kuzingatia maneno hayo ya Mwasisi wa Taifa. Kitendo cha wasomi kupendelea ajira za ofisini na kususia kilimo kunaweza kuzorotesha maendeleo ya sekta ya kilimo ambayo ni mwimo wa sekta nyingine. Chakula na bidhaa za kilimo ndiyo maisha hivyo ni bora taifa likawekeza elimu kubwa katika kupata wakulima wenye elimu ya uzalishaji wa mazao na mifugo kwa taifa imara.

Kwa kuzingatia hilo serikali ya awamu ya kwanza chini ya uongozi wa Rais Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alianzisha Shule ya Mahiwa na tarehe 15 Julai, 1964 alisema; "hii ni Shule ya maana sana. Msingi wake ni ile imani kwamba vijana waliomaliza Elimu ya Msingi wanayo nafasi yao ya kushiriki katika maendeleo ya nchi, wakiwa wakulima hodari na wenye elimu. Hapa watajifunza ukulima wa kisasa, watajifunza elimu hii ili waweze kuitumia mara moja nchini. Ndiyo kusema kuwa mkazo wa masomo utakuwa juu ya kutumia vifaa vinavyoweza kupatikana na kutumiwa katika Jamhuri ya Muungano."

‘Litatiliwa mkazo vile vile somo la kutunza rutuba ya ardhi na kuzuia mmomonyoko wa udongo, mambo hayo mawili ambayo ni muhimu sana kwetu. Zaidi ya hayo, masomo ya hapa yatatiliwa mkazo vyama vya ushirika kuwa ni njia ya kuondoa tatizo la uuzaji wa mazao. Wanafunzi watakaohitimu hapa wataweza kutimiza wajibu wao barabara katika maendeleo ya vijijini.”

Halikadhalika alizungumzia azimio la elimu ya kilimo kwa watu wazima yaani wakulima ili kila mmoja aelimike kulingana na tatizo lake.

Swali la kujiuliza, hadi sasa ni zaidi ya nusu karne tangu mwenge wa uhuru uwashwe, na Tanganyika kuwa Jamhuri. Je, ipo mitaala ya kufundishia wakulima kuhusu uzalishaji wenye tija kama ilivyofikiriwa kwenye mipango ya viongozi wa nchi na serikali?

Ni jukumu la wataalamu kuhakikisha haya yanatekelezeka kama hotuba ya mwezi Machi, 1967 (mswada) wa elimu ya kujitegemea ilivyofafanua. Rais wa awamu ya kwanza, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alisema;

“Tangu siku nyingi kabla ya uhuru watu wa nchi hii, chini ya uongozi wa TANU, wamekuwa wakidai elimu zaidi kwa watoto wao. Lakini bado hatujakaa na kufikiri kwa nini tunataka elimu, na ina shahada gani? Kwa hiyo, ingawaje kwa siku nyingi mafunzo yanayotolewa katika shule yametolewa makosa, lakini mpaka sasa hatujaitoa makosa misingi yenyewe ya elimu tuliyoirithi wakati tulipopata uhuru wetu. Hatujafanya hivyo kwasababu

hatujafikiria bado habari ya mipango ya elimu, isipokuwa katika kupata walimu, mainjinia, mabwana shauri na wengineo."

"Kila mtu binafsi na hata sote kwa pamoja tumefikiria elimu kama mafunzo ya kazi ya kujipatia mishahara mikubwa katika kazi za kisasa," (Nyerere, 2004).

## Elimu ya kikoloni;

*Chanzo cha dharau na matabaka ambacho Mwenge wa Uhuru ulitakiwa kushughulika nao ni kama ifuatavyo;*

"Elimu iliyokuwa ikitolewa na serikali ya mkoloni katika nchi zile mbili; Unguja na Tanganyika, ambazo sasa ni Tanzania ilikuwa na shahada tofauti. Haikupangwa ili kuwaandaa vijana kutumikia taifa lao; badala yake ilipangwa kwa kutimiza haja za kuingiza desturi za kikoloni. Kwahiyo, haja ya elimu katika nchi hizi ilitokana na haja ya kuwa na makarani na maofisa wa vyeo vya chini. Vilevile vikundi mbalimbali vya dini vilitoa mafunzo ya kusoma na kuandika na elimu nyingine kwa njia ya kueneza imani yao," (Nyerere, 2004). Bishop G, (1985), aliwahi kumnukuu Prof. Abdou Moumouni wa Niger katika kitabu chake kinachoelezea masuala ya mitaala ya Elimu kiitwacho "CURRICULUM DEVELOPMENT" alisema; "Schools which bear no relationship to their surroundings, schools which are cut off from the life of the country and society, ….unproductive schools which only train pupils for the civil service, which destroy national cultural values and

personality and produce men who are foreigners in their own society."

Mwalimu J.K Nyerere aliendelea kusema kuwa; "Shahada ya kuuhitaja ukweli huu siyo kukashifu wale wengi waliofanyakazi ngumu, mara nyingi kwa shida kubwa katika kufundisha na kuweka mipango ya elimu. Wala sisemi kwamba yote waliyoyafundisha shuleni yalikuwa ya kupotosha na yasiyofaa. Ninachosema ni kwamba; elimu iliyotolewa na mkoloni katika Tanzania ilikuwa na mtindo wa Kiingereza, lakini mkazo wake wa fikra za ubwana na kufanyakazi za ofisini ulikuwa mkubwa zaidi hata kuliko ilivyokuwa kule Uingereza. Kadhalika elimu hiyo ilikuwa imepangwa kwa mtindo wa kikabaila. Ilitilia mkazo fikra za kila mtu kuishi peke yake badala ya mawazo ya kushirikiana. Iliwafanya watu wafikiri kwamba dalili ya heshima ya mtu katika taifa ni kujilimbikizia mali nyingi," (Nyerere, 2004).

*Kwa kuwa elimu ya kikoloni iliwafanya Watanzania kuwa na matabaka yaani wenye nacho na wasionacho ndipo Mwalimu J. K Nyerere alipoweka mpango mkakati wenye kufanyakazi kila mwaka yaani mwenge wa uhuru unaokimbizwa kwa ukakamavu nchi mzima. Ili kusafisha matendo yaliyozalishwa na elimu ya mtindo wa kikoloni na* ***kuleta tumaini*** *kwa Wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyojifafanua katika tamko la mwasisi wa Mwenge wa uhuru ya kuwa;*

"Ndiyo kusema kwamba elimu ya kikoloni ilileta fikra za mtu kuwa bwana na wengine watwana, na kwa kweli

iliwafanya wanyonge wakandamizwe na wenye nguvu, hasa matajiri. Kwa hiyo elimu ya kikoloni katika nchi hii haikuwa ya kuendeleza ujuzi na mila za Watanzania kutoka kizazi kimoja hadi kingine; ilikuwa na juhudi hasa ya kubadili mawazo hayo na badala yake kupanda mila na ujuzi kutoka nchi nyingine." Aliendelea kusema; "Na hivyo ilikuwa sehemu ya juhudi ya kuleta mapinduzi ya mawazo katika nchi; kuyageuza yawe ya watu wa kikoloni wanaokubali hali hiyo mawazo yatakayokuwa ya msaada kwa serikali inayotawala. Pengine hawakufaulu katika shahada hiyo, lakini hiyo siyo kusema kwamba wameshindwa kugeuza fikra, tabia ya wale waliopitia shule zao. Wala kushindwa huko maana yake siyo kusema kwamba elimu iliyotolewa enzi ya ukoloni ilikuwa na shahada ya kuwalea watu wanaoamini usawa wa binadamu." '……..kwa kweli nchi huru ya Tanzania ilirithi mtindo wa elimu ambayo kwa njia nyingi ilikuwa haitoshi wala haifai kwa haja za nchi hii. Elimu yetu haina budi ipande mbegu ya watu kuishi pamoja na kufanya kazi pamoja kwa faida ya wote," (Nyerere, 2004).

*Kuna uwezekano mkubwa waurithi huu wa elimu ya kikoloni, kuwa ndiyo unaozalisha ufisadi miongoni mwa wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*

Watu wengi walibeza mawazo ya Mwalimu J. K Nyerere yaliyotaka wananchi wote kuishi kijamaa, ingawa alilitolea ufafanuzi katika hotuba zake na kusema; "Ujamaa sio lazima iwe kuishi kama ndugu kwa kula sahani moja ya chakula badala yake kila mwananchi kuwa mzalendo kwa

kufanyakazi kwa manufaa ya taifa zima badala ya kipato cha familia ya mtumishi," (Nyerere, 2006).

Kupitia kauli mbiu za mbio za mwenge wa Uhuru, wananchi wa Tanzania waliweza kuelimishwa kuhusu elimu ya kujitegeme na uzalendo.

**Elimu baada ya uhuru;**

Matumaini yaliyoletwa baada ya uhuru; ni kuondoa makosa matatu makubwa yaliyorithiwa toka kwenye elimu ya kikoloni nayo ni: *mosi***,** ubaguzi wa rangi.  Ubaguzi wa rangi katika kugawa elimu ulifutwa mara tu baada ya Uhuru, na ubaguzi kutokana na dini pia ulikomeshwa. *Pili*, nafasi za masomo zimeongezwa, hasa katika Shule za Sekondari na za Vyuo vya juu. *Tatu***,** ni kuifanya elimu inayotolewa katika shule zetu zote iwe ya ki-Tanzania zaidi katika muundo wake.

"….Watoto wetu sasa hawajifunzi historia ya Kiingereza na Ulaya peke yake. Kwa haraka zaidi kuliko tulivyodhania imewezekana *Chuo chetu Kikuu na Vyuo vingine kutoa vitabu vya historia za Kiafrika na kuwapa walimu wetu*. Watoto wetu wamerudia kufundishwa nyimbo na ngoma zetu za Taifa. Lugha yetu ya Taifa (Kiswahili) inatiliwa mkazo unaostahili katika masomo. Kadhalika, mafunzo ya uraia yanaanza kuwapa nafasi wanafunzi wa Shule za Sekondari kuelewa muundo na shabaha za Taifa letu changa. Kwa njia hizi na nyingine, yameletwa mabadiliko kufanya mtindo wetu wa elimu ufanane na haja zetu. Kwa wakati huu ambapo watu wanadadisi kazi zinazofanywa

(na haki yao waulize), inafaa tushukuru kazi inayofanywa na walimu wetu na wale wanaoangalia kazi yao katika Wizara, katika Chuo cha ualimu, katika Chuo kikuu na Halmashauri za wilaya," (Nyerere, 2004).

Miaka zaidi ya 50 baada ya uhuru na miaka 20 baada ya kifo cha Baba wa taifa; idadi ya wasomi wa Kitanzania waliopata elimu ya juu imeongezeka kwa kiasi kikubwa, vyuo vikuu nchini vimekuwa vingi lakini hadi sasa bado nchi ni maskini. Uchumi wake mkubwa unategemea kilimo lakini wakulima walio wengi wanatumia jembe la mkono. Mwenge wa uhuru mulika na huku!

Muda umefika wakufuatilia hotuba za Baba wa taifa ili kupata taifa jipya kama hotuba hii inavyojieleza kwenye kitabu kiitwacho "NYERERE KUHUSU ELIMU, SELECTED ESSAYS AND SPEECHES 1954 - 1998", "Tukifahamu barabara aina ya taifa tunalotaka kulijenga, ndipo tutakapoweza kuweka mipango ya elimu yenye kutufikisha kwenye shahada hiyo."

***Umulike***; "Hata hivyo ni dhahiri kwamba, kama tunataka kupiga hatua kuelekea lengo hilo, sisi watu wa Tanzania hatuna budi tukubali hali yetu ya ndani ya nchi na hata nje, halafu tufanye bidii kuibadilisha hali hiyo ilingane na shahada yetu. Na kweli kwamba Jamhuri yetu ya Muungano hivi sasa ni maskini, haijaendelea na uchumi wake mkubwa ni kilimo. Hatuna rasilimali ya kutumia; tuna upungufu mkubwa wa watu wenye stadi na uwezo wakuendesha viwanda vikubwa au mashine za kisasa. Vitu tulivyonavyo ni ardhi kwa wingi na watu walio radhi

kufanyakazi kwa bidii kujiinua hali zao, kufika ama kutofika katika lengo letu kunategemea tu matumizi yetu ya vitu na vitu hivyo viwili, ardhi na watu. Kama tutatumia amali hizo kwa moyo wa kujitegemea kuwa ndiyo msingi wa maendeleo yetu, basi tutapiga hatua yenye uhakika, ingawa kwa taratibu. Hayo ndiyo yatakayokuwa maendeleo ya kweli, yatakayoleta faida katika maisha ya umma na siyo maendeleo ya maonesho tu katika miji, wakati watu wote wengine wa Tanzania wanaishi maisha yale yale ya ufukara tulio nao sasa."

***Matumaini***; "Kwa kweli nchi huru ya Tanzania ilirithi mtindo wa elimu ambayo kwa njia nyingi ilikuwa haitoshi wala haifai kwa haja za nchi hii. Lakini kulikodhihirika mapema zaidi ni kutokutosha kwa elimu." *Elimu iliyotolewa ilikuwa kidogo mno. Kauli hii ilielekezwa katika mambo mawili nayo ni; kutosha kwa idadi ya wasomi wa kitanzania*. "Desemba 1961, watu wenye elimu ya kutosha walikuwa wachache mno wala wasingetosha kuendesha serikali ya siku zile, wacha kazi zingine za mipango ya maendeleo zilizokuwa muhimu zaidi. Wala idadi ya watoto waliokuwa shuleni mwaka huo haikuwa kubwa ya kutoa matumaini kwamba hali hii ingeweza kurekebishwa haraka," (Nyerere, 2004).

*Lakini pia kutotosha kwa maana ya ubora wa elimu iliyotolewa kwa Watanganyika kwa kuwa ilitolewa kwa ubaguzi kama ilivyoelezwa katika ripoti ya Rais Julius Kambarage Nyeree mwaka 1967*; "Elimu iligawiwa kwa mataifa, ambapo msingi wa madai yetu yote ya uhuru

ulikuwa ni kulaani kabisa ubaguzi wa rangi," (Nyerere, 2006).

Kwa sasa Tanzania hakuna ubaguzi wa rangi lakini elimu inayotolewa kwa watoto nchini sio ya kibaguzi? Ikiwa kuna shule zinazotumia lugha ya Kiingereza kwa mawasiliano na kufundishia kwa wanafunzi wao tangu elimu ya Awali wakati wengine wanatumia lugha hiyo kujifunzia tu. Tabaka la wanafunzi hawa linakuja kuonekana wafikapo kwenye soko la ajira. Hivyo ni jukumu la wataalamu wa masuala ya elimu kuwezesha mipango itakayofaa ili kuwepo na elimu itakayoipeleka nchi kwenye mabadiliko ya kweli kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania wote.

Maxwell katika kitabu chake cha "LAWS OF LEADERSHIP" aliwahi kusema kwa masikitiko; "Major barrier to successful planning are fear of change, ignorance, uncertainty about the future, and lack of imagination." Kwenye kutafuta mwarobaini wa jambo hili, kuna watu wanaamua kwenda ng'ambo kusaka elimu wanayohisi imeboreshwa. Wakati Lee Kuan, (2000) aliyepata elimu yake ya juu Ulaya na kuwa kiongozi wa ngazi za juu nchini kwao, aliandika namna elimu ya ugenini ilivyokuwa na madhara katika utamaduni wa jamii uliyotoka. Alisema kwa masikitiko kuwa; "when we met students from China while studying in England, we became conscious of how deculturalised we were, almost like the Chinese students from the Caribbean."

# HISTORIA YA MWENGE NA UCHAWI

Siku hadi siku katika miongo ya karibuni kumeibuka kundi la wananchi wanaouchukia mwenge wa uhuru. Sababu yao kubwa ya kuupinga mwenge wa uhuru pamoja na mbio zake ni;

1. Mwenge wa uhuru unatukuza imani za kichawi.
2. Usambazaji wa virusi vinavyosababisha UKIMWI yaani VVU katika mikesha ya mbio za mwenge wa uhuru.
3. Itikadi za kisiasa na vyama vya siasa
4. Bajeti kubwa ya mbio za mwenge wa Uhuru zinazopelekea wananchi kuchangishwa michango ya lazima.

## Mwenge wa Uhuru na uchawi

*Historia*

Kabla ya mkutano wa Berlin kulikuwa hakuna taifa lenye jina la Tanganyika badala yake kulikuwa na maeneo madogo madogo ya kikabila yaliyoongozwa na Machifu. Mwaka 1886, maeneo yote yaliyopatikana Mashariki mwa ziwa Tanganyika hadi Pwani ya Bahari ya Hindi yaliunganishwa na kuwa koloni la Kijerumani kwa jina la

**Tanganyika** kutoka kwenye jina la Afrika ya Mashariki ya Kijerumani, (Rai, 2016).

Wahenga husema; *anayesifia uchawi wa mwenzie basi na yeye mchawi*. Hivyo kuna wachawi wanaosema; "Mwenge wa uhuru na uchawi ni kama pande mbili za shilingi." Kwa sababu; Kabla ya mwenge wa uhuru kuwashwa, Mwalimu Nyerere aliwashirikisha wachawi maarufu wakiongozwa na mchawi mkuu kwa jina Forojo Ganze kufanya zindiko kama ilivyoelezwa na (Kagasheki, 2016), "zindiko lilifanywa Bagamoyo katika moja ya mapango maarufu katika Pwani hiyo. Washiriki waliofanikisha zoezi hilo ni Wazee wa Dar-es-salaam, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, wazee wa Bagamoyo, viongozi wa kichifu (Machifu) kutoka maeneo mbalimbali na wafuasi wa Forojo Ganze. Ganze alifariki dunia muda mfupi baada ya zindiko hili kufanyika" (Kagasheki, 2016).

Lengo la zindiko lililoelezwa na wachawi ni; "kuhakikisha Rais aliyemadarakani (Mwalimu J. K Nyerere) hapingwi na mtu yeyote sambamba na kuuliza shetani juu ya jambo gani lifanyike ili Tanzania iendelee?" (Kagasheki, 2016). Wapinga mwenge waliendelea kueleza ya kwamba maneno yaliyotamkwa na Mwalimu Nyerere yaani "tunauwasha mwenge na kuuweka mlima Kilimanjaro na umulike hata nje ya mipaka yetu ili ulete; tumaini pale ambapo hakuna matumaini, upendo mahali palipo na chuki na heshima palipojaa dharau." Ni maneno aliyoyatamka Forojo Ganze kama kauli yake ya mwisho siku ambayo alitoka pangoni baada ya kukaa huko kwa

muda wa siku kumi kisha akakata roho, (Kagasheki, 2016). Mambo haya yanaelezwa kuwa yalitokea mwaka 1961.

Kwa upande wa pili historia ya mwenge wa uhuru ilihusu Tanganyika sio Tanzania pia kauli ya mwenge ilitamkwa kabla ya kufanyika kwa tambiko yaani Mwalimu Nyerere aliazimia kuuwasha mwenge akilihutubia Baraza la kutunga sheria tangu mwaka 1959, miaka miwili kabla ya uhuru. Hata hivyo, mwaka 1961 wakati Mwenge wa uhuru unawashwa; taifa la Tanganyika halikuwa na Rais wa Kiafrika sababu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikuwa ni Waziri Mkuu hadi baada ya uchaguzi wa mwaka 1962 ndipo Tanganyika ilipokuwa Jamhuri na Mwalimu J.K Nyerere kusimikwa kuwa Rais wa kwanza wa Tanganyika.

**Uchawi ni nini**? (Witchcraft)

*Uchawi* ni ufundi wa kutumia dawa au maandishi maalum ya uganga ili kuleta madhara kwa viumbe, (TUKI, 2004). *Uchawi* ni nguvu zinazotumiwa na watu wenye maarifa maalum yasiyo ya kisayansi katika jamii nyingi duniani, ingawa kuna tofauti kulingana na mahali, au utamaduni. Lengo la uchawi (kuloga) ni kujaribu bahati, kujilinda, na maadui kimazingara, au kwa ajili ya kujifurahisha.

Tangu uhuru, serikali ya Tanzania inajitahidi kuelimisha wananchi kuhusu imani potofu na uchawi ambavyo hupelekea migogoro miongoni mwa wanajamii au familia. Wakati mwingine husababisha vifo au mauaji ya vikongwe

kama ambavyo iliwahi kuripotiwa kwenye vyombo vya habari kuwa; mikoa ya Shinyanga, Kigoma, Tabora, Dodoma na Mara yalitekelezwa matukio ya mauaji ya aina hiyo. Matukio mengine ya kikatili yanayohusishwa na imani za kishirikina ni kuchomwa moto nyumba za watu wanaohisiwa ni wachawi kwa lengo la kuwadhalilisha na kuwanyanyapaa. Pia miongo ya karibuni yaani Mwanzoni mwa karne ya 21; maeneo mbalimbali nchini kulishamili mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi (Albino) pamoja na kukatwa baadhi ya viungo kwa imani za kichawi.

Hadi kufikia mwaka 2008, Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alilaani mauaji hayo ya kichawi na kusema; “mtu atakayebainika kwa namna yeyote ile achukuliwe hatua za kisheria, kwa sababu mauaji ya Albino huzua taharuki katika jamii," (Wikipedia).

**Ushirikina (**Superstition**)**

TUKI, (2004), ushirikina ni tabia ya kuamini mambo ya ramli na uchawi.

**Utamaduni (**Culture**)**

Utamaduni ni mila, desturi, asili, jadi, imani na itikadi za kundi la watu au jamii fulani (TUKI, 2004). *Utamaduni* ni jinsi binadamu anavyokabili maisha katika mazingira yake. Inajumlisha ujuzi, imani, sanaa, maadili, sheria na desturi ambavyo mtu anajipatia kama Mwanajamii, (Wikipedia). *Utamaduni* ni jumla ya mambo yote yanayobuniwa na

jamii ili kukidhi utashi na maendeleo yake. Au *utamaduni* ni mwenendo wa maisha ya jamii, mtazamo wao wa mambo, na taratibu zao za kuendesha maisha zinazowatofautisha wao na jamii nyingine, (MOEC, 1997).

**Mila**

Ni mambo yanayofanywa na jamii ya watu kwa mujibu wa asili na utamaduni wao, (TUKI, 2004). Mila ni mambo yanayofanywa na jamii fulani ambayo yanalingana na asili, mazingira na nyendo za jamii hiyo. (Mojasky, 2019)

**Desturi** (Custom)

*Desturi* ni jambo ambalo mtu hulifanya kama kawaida au kanuni (TUKI, 2004). Mfano mbio za mwenge wa uhuru kila mwaka kukimbizwa nchi mzima ni desturi. Pia Mojasky, (2019) ameeleza; *desturi* ni jambo la kawaida linalotendwa kila siku

**Tambiko**

*Tambiko* ni ibada ya kutuliza mizimu au pepo au kuomba msaada wao.

**Zindiko**

*Zindiko* ni dawa ya kienyeji inayowekwa mahali fulani kwa mfano nyumbani, shambani au dukani ili kuzuia madhara (TUKI, 2004).

Shughuli hii hufanywa na waganga wa jadi au wachawi, hivyo wanatumia mizimu, majini, mashetani, na dawa ili

kuweka ulinzi huo usioonekana. Tatizo ni kwamba; unakuwa na ulinzi wenye mkataba wa siri kati ya nguvu hizo na mganga hivyo ni rahisi kukosea masharti na kupelekea kudhuru watu au mhusika mwenyewe hasa kwa mazindiko ya muda mrefu.

*Hivyo kwenye mwenge wa uhuru inawezekana kusiwe na uchawi na kukawa na zindiko*. Shughuli nyingi za kijamii Barani Afrika zinaambatana na mazindiko ili kuzuia madhara yatayosababishwa na mkusanyiko mkubwa wa watu.

Mbio za mwenge wa uhuru zinahusisha mikusanyiko ya watu, misafara ya magari, maandamano na mikesha. Iwapo sherehe za unyago na ndoa zinafanyiwa mazindiko ya ulinzi ili kuepusha madhara kwa wahudhuriaji wa shughuli hiyo, sasa itoshe kusema mazindiko ni mila na desturi ya jamii za Watanzania. Endapo Wazee walikusanyika mwaka 1961 mjini Bagamoyo na kufanya tambiko kuhusu Mwenge wa Uhuru, kuna uwezekana mkubwa kuwa waliweka zindiko ili kuepusha madhara na sio kupumbaza akili za wananchi wa Tanzania.

## MKESHA WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU

Usambazaji wa virusi vinavyosababisha UKIMWI yaani VVU katika mikesha ya mbio za mwenge wa uhuru.

**Nini maana ya mkesha?**
MKESHA kutoka kwenye tafsiri ya lugha ya Kiingereza "vigil" lenye asili ya Kilatini kwa neno la "vigilia" ni hali ya kuwa macho (Wikipedia). Mkesha ni siku inayotangulia siku yenye shughuli maalum kwa mfano mwaka mpya (TUKI, 2004). Katika jamii za Kitanzania mkesha hufanyika kwenye shughuli kama vile ndoa, jando na unyago, matambiko, na hata kuwa macho kando kando ya mgonjwa aliyemahututi au maiti.

Mkesha wa mwenge wa uhuru hufanyika mara moja katika kituo kimoja kila wilaya nchi mzima kwa mwaka. Mkesha huu unahusisha viongozi wa mkoa na wilaya husika, wananchi pamoja na vyombo vyote vya ulinzi na usalama kuhakikisha shughuli inakamilika kama ilivyopangwa.

Licha ya mkesha wa mbio za mwenge wa Uhuru, nchini Tanzania kuna mikesha mingine. Wakazi wa Ukanda wa Pwani wanashughuli nyingi zinazowavuta wakazi wa maeneo hayo kukusanyika na kukesha. Mfano kuna muziki wa hadhara alimaarufu 'kigodoro', ngoma za asili zinazopigwa nyakati za furaha hasa katika msimu wa mavuno katika kila kabila. Pia shughuli za ndoa nchi mzima kwa mfano mafundo, mwago, na shughuli ya ukumbini inayofanyika siku ya ndoa, zote zina mkesha. Lakini hata maadhimisho ya sikukuu za kidini kama vile

usiku wa Maulidi, mkesha wa mwaka mpya, na mkesha wa Krismasi nazo watu hukesha.

Shughuli nyingine zinazowafanya watu kukesha ni pamoja na shughuli za huzuni kama misiba na matanga. Pia kuna jamii nyingine zina mila ya kutambikia mizimu kila mwaka na ngoma za asili. Kwenye vilabu vya pombe, kumbi za starehe na shughuli za michezo huko nako watu wanakesha.

Wahenga husema; "kila penye heri, hapakosi shari." Katika mkesha kusudi ni kukamilisha malengo ya shughuli iliyoandaliwa lakini kuna watu wanajumuika kwa makusudio yao binafsi. Badala ya kukesha akiabudu, mtu huyo anaweza kufanya uzinzi, watu wengine wanaomboleza lakini kuna mtu anatumia fursa na kuona ndiyo muda mwafaka wa kwenda mchepuko. Wapo baadhi ya watu wazima wanaokwenda shughulini iwe kwenye mkesha wa mwenge wa uhuru au ngoma, kwa lengo la kubaka watoto wanaowatoroka wazazi wao nyumbani usiku. Miongoni mwa watoto hao ni wanafunzi wa Shule za Sekondari au Shule za Msingi, au kuwabaka watu wenye ulemavu wa akili.

Hivyo kama kweli mkesha unaweza kusababisha madhara makubwa ikiwemo kuwa chanzo cha kusambaa kwa VVU na mimba za utotoni, basi watu wakubali kukataa mikesha yote inayoendeshwa katika maisha ya kila siku. Lakini ikionekana mkesha unaweza kuwajenga watu kiimani, kudumisha amani, upendo, mshikamano, kuleta furaha, kutoa elimu ya maisha, kufarijiana na mambo mengine

 © 2020

yenye manufaa yanayoletwa na mkesha achilia mbali madhara machache yatokanayo. Watu wakubali kuwa mkesha ni sehemu ya maisha yeo bila kubagua ni mkesha wa mwenge wa uhuru au shughuli nyingine ya kiuchumi, kijamii, itikadi, au kidini.

## Hali ya UKIMWI

Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI) ni ugonjwa unaosababishwa na upungufu wa kinga ya mwili (TUKI, 2004). Kwa Kiingereza Human Immunodeficiency virus (HIV) ugonjwa unaotokana na virusi (VVU) vinavyoshambulia mwili kwa kuondoa nguvu zake za kupambana na maradhi (RFI, 2018).

Taarifa ya Shirika la Afya Duniani ilieleza; "hadi kufikia mwaka 2014, UKIMWI umeua watu milioni 39 hasa kwa wakazi wanaoishi katika nchi zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara. Kufikia mwaka 2015, wamefariki watu milioni 1.2 na wengi wao ni watoto. Ugonjwa huu uligunduliwa nchini Tanzania mnamo mwaka 1983” (RFI, 2018).

*Chapisho la RFI la tarehe 26 Julai, 2018 lilieleza namna mtu anavyoambukizwa HIV;*

1. Njia kubwa ni kushiriki ngono na mtu aliyeathirika.
2. Kuchangia vifaa vyenye ncha kali kama sindano na mtu aliyeathirika.
3. Kuongezewa damu kutoka kwa mtu aliyeathirika (kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine).
4. Kutoka kwa mama aliyeathirika hadi kwa mtoto wakati wakujifunga.

**Sababu za kuongezeka kwa maambukizi ya Virusi vya Ukimwi**

**Tabia**; Utafiti uliofanywa na mashirika mbalimbali kama WHO Barani Afrika, unaonesha kuwa watu wanaojihusisha katika ngono na zaidi ya mpenzi mmoja, wapo katika hatari kubwa ya kupata maambukizi (RFI, 2018).

**Hali ngumu ya Kiuchumi;** kutokana na ugumu wa maisha, wanawake wengi hasa wasichana huamua kujiuza ili kujipatia kipato.

**Kutahiri na Kukeketa**; kutahiri wanaume na kukeketwa kwa wanawake kwa njia ya kitamaduni hasa Barani Afrika kama vile nchini Kenya, Lesotho na Tanzania kumeendelea kuhatarisha maisha ya watu wengi.

**Matumizi yasiyosahihi ya mipira ya kujikinga na virusi (condoms)**
Ngono bila kutumia kinga, kuwa na wapenzi wengi, na matumizi ya kondomu kwa kiwango kidogo na kisichoendelevu ni moja kati ya vyanzo vikuu vya maambukizi mapya (BBC, 2019).

Imewahi kuripotiwa na BBC Swahili katika chapisho lao la tarehe 21 Februari, 2019, kuhusu upandaji wa bei za kondomu mkoani Njombe na kusababisha taharuki kwa watumiaji. Bei ya bidhaa hiyo ilipanda kutoka kati ya Tsh.500-1000 kwa paketi yenye kondomu tatu hadi Tsh. 1,500 - 2,500 kulingana na sampuli za kondomu hizo.

Naibu Waziri wa Afya, Dkt Faustine Ndugulile alitolea maelezo kuhusu kupanda kwa bei ya bidhaa hiyo; "kuwa kondomu zilizokuwa zinatolewa bure ama kwa bei nafuu zimeadimika. Hali hiyo imetokana na mabadiliko katika mifumo ya usambazaji wa kondomu. Utaratibu wa awali; serikali pamoja na baadhi ya mashirika binafsi nchini yalikuwa yakipata ruzuku kutoka kwa taasisi ya Afya ya Global Fund. Badala yake awamu hii ruzuku hiyo wamepatiwa serikali pekee. Hivyo Wizara ya Afya ndiyo itakuwa inasimamia uingizwaji wa kondomu. Kwahiyo changamoto imefanyiwa kazi na kondomu zimeanza kusambazwa," (BBC, 2019).

Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI kwa nchi ni 4.7% lakini kwa mkoa wa Njombe wastani wa maambukizi ni 11.4%.
Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kasimu Majaliwa alifafanua viwango vya maambukizi ya Virusi vya UKIMWI nchini kuwa bado ni vikubwa kwa mujibu wa utafiti wa nne uliofanyika katika ngazi ya kaya kwa mwaka 2016 hadi mwaka 2017. Aliyasema hayo Jijini Dar-es-salaam mwezi Mei, 2018 wakati akizindua Mkakati wa Maadhimisho ya miaka 15 tangu kuanzishwa kwa Mfuko wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Kupambana na Kudhibiti Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (PEPFAR).

Katika hotuba ya Waziri Mkuu alieleza; "Tanzania watu takribani milioni 1.4 wanakadiriwa kuishi na virusi vya UKIMWI. 81,000 hupata maambukizi mapya ya virusi vya

UKIMWI kila mwaka na waathirika wakubwa ni wasichana" (DodomaFM, 2018).

*Mikoa iliyotajwa kuwa inaongoza kwa kiwango kikubwa cha maambukizi juu ya wastani wa kitaifa wa 4.7% kuwa ni;*

| | |
|---|---|
| Njombe | 11.4% |
| Iringa | 11.3% |
| Mbeya | 9.3% |
| Mwanza | 7.2% |
| Kagera | 6.5% |
| Katavi | 5.6% |
| Shinyanga | 5.9% |
| Dodoma | 5.0% |

Pia, katika hotuba ya Waziri wa fedha na Mipango Dkt. Philip Mpango Desemba, 2017 akiwa anamkabidhi Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli takwimu ilionesha hali ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI (VVU), wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi katika ofisi za Takwimu jijini Dodoma alisema; "Mikoa yenye ongezeko kubwa la watu wanaoishi na maambukizi ya virusi vya UKIMWI ni Mkoa wa Mwanza, Tanga, Kagera, Dodoma, Manyara na Iringa. Wakati mikoa yenye maambukizi ya kiwango cha chini ni Unguja 0%, Kaskazini Pemba 0%, Lindi 0.3%, Manyara 1.8% na Arusha 1.9%." Takwimu imetokana na utafiti uliofanywa na ofisi ya Takwimu ya Taifa juu ya hali ya maambukizi kwa watu wenye umri wa miaka kati ya 15-49 kwa mwaka 2016-2017 (Zanzibar24, 2017).

Mkurugenzi wa TACAIDS Dkt. Leonard Maboko katika mahojiano na Mwandishi wa Gazeti la Rai lililochapishwa tarehe 25 Julai, 2019 alisema; "Zaidi ya Dola za Marekani bilioni 26.2 zinahitajika katika juhudi za kupambana na ugonjwa wa UKIMWI hapo mwakani (2020) kutoka Dola bilioni 19 zilizotolewa mwaka jana. Sababu maambukizi yanatajwa kuongezeka zaidi miongoni mwa watu wasiopata huduma za kuepusha maambukizi na kuonesha kuwa fedha zaidi zinazohitajika ili kutoa huduma za kupambana na ukimwi."

Kauli ya kiongozi huyo kuhusu namna ya kupunguza maambukizi alisema; "Mambo yatakayoleta heri nchini kuhusu ugonjwa wa UKIMWI ni kuhakikisha Watanzania wote bila kujali dini, kabila, itikadi za kisiasa ama rangi zao, wanashiriki kuutokomeza ugonjwa huu" (Rai, 2019).
Wakati zinahitajika Dola za Marekani bilioni 26.2 kwa ajili ya mapambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI mwaka 2020, kuna janga jingine jipya la kidunia limetokea. Ugonjwa wa CORONA (COVID-19) na kusababisha kusimama kwa shughuli za uzalishaji mali na kusababisha vifo vya watu wengi duniani. Je, tutaendelea kupambana na UKIMWI au CORONA ama vyote?

## ITIKADI ZA KISIASA NA VYAMA VYA SIASA

Wananchi wengi wa Tanzania wanaamini mwenge wa uhuru ni wa Chama cha Mapinduzi na serikali yake iliyopo madarakani na sio mwenge wa Wananchi. Hivyo kutoona umuhimu wa uwepo wake na kutamani kufutwa kwa kumbukumbu hiyo.

Tarehe 12 Februari, 2010, Mbunge wa Manyoni Magharibi Mhe. John P. Lwanji katika kipindi cha maswali na majibu bungeni aliwahi kumuuliza Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana; swali linaloweka bayana undani wa jambo hili.

*Majadiliano yalikuwa kama ifuatavyo; Mbunge wa Manyoni Magharibi, Mhe. John P. Lwanji aliuliza,*

(A). Je, ni utaratibu gani na vigezo gani vinavyotumika katika kuwateua vijana wanaokimbiza mwenge?
(B). Je, vijana hao wanapata posho kiasi gani kwa siku na kuna malipo yoyote wanayopewa baada ya kumalizika kwa kazi ya mbio za mwenge?

(C). Je, vijana hao hulipwa nini pindi wanapopatwa na ajali wakati wakikimbiza mwenge?

**Majibu ya Waziri wa kazi, ajira na maendeleo ya vijana;**
(A). Kwa mwongozo wa mbio za mwenge, utaratibu wa kuwapata wakimbizi wa mwenge kitaifa ni kama ifuatavyo;

I. Mwenge wa uhuru kitaifa hukimbizwa na vijana sita, kati ya vijana hawa mmoja huchaguliwa kuwa kiongozi. Kiongozi wa mbio za mwenge huchaguliwa kwa zamu kutoka Tanzania bara mwaka mmoja na mwaka unaofuata Tanzania visiwani. Aidha, uteuzi wa Wakimbiza mwenge unazingatia kwamba jinsia zote zinashiriki. Mikoa inayoanzia au kumalizia mbio za mwenge hutoa mkimbiza mwenge kila mwaka.

II. Wakimbiza mwenge huchaguliwa kutoka kwenye majeshi, taasisi za serikali, vyama vya hiari ama vikundi vya vijana vya uchumi.

III. Maombi ya wakimbiza mwenge watatu (3) yanatoka mikoa inayozindua na kuhitimisha mbio za mwenge. Yatapitishwa na kamati ya ulinzi kabla ya kuwasilishwa Wizarani kwa uteuzi.

IV. Wakimbiza mwenge kutoka Zanzibar huteuliwa huko huko Zanzibar na majina huletwa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana.

 © 2020

*Vigezo vinavyotumika kuwapata wakimbiza mwenge ni pamoja na vijana wanaoomba kukimbiza Mwenge kuwa na sifa zifuatazo;*

i. Watanzania wenye umri kati ya miaka 18-35.

ii. Wawe na Afya njema, tabia njema na akili timamu.

iii. Wawe na elimu ya kidato cha nne au zaidi na wenye ufahamu wa masuala mbalimbali ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

iv. Wawe na uwezo wa kujieleza mbele ya wananchi.

v. Wawe na uwezo wakufaulu mafunzo yatakayotolewa ikiwa ni pamoja na uwezo wa kumudu mazoezi ya viungo na nadharia wakati wa maandalizi.

vi. Wawe na nia ya dhati ya kujitolea kukimbiza mwenge na wakubaliane na masharti ya uendeshaji wa shughuli za mbio za mwenge.

(B). Kazi ya kukimbiza mwenge wa uhuru dhana yake hasa ni ya kujitolea. Hata hivyo, wakimbiza mwenge hulipwa posho kwa siku kwa ajili ya matumizi ya mahitaji madogo madogo yanayoweza kujitokeza katika safari hiyo. Wizara sasa hivi inapitia posho hizi ili ikiwezekana zirekebishwe kulingana na mahitaji na gharama za sasa.

(C). Kutokana na umuhimu wa shughuli hii, vijana wanapopatwa na ajali wanalipwa bima. Hivyo Wizara huhakikisha kwamba vijana wamepata kinga ya bima ya ajali kabla ya kuanza mbio za Mwenge, (Bunge, 2010).

*Mhe. Lwanji alipata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo;*
"Kumekuwa na malalamiko kwamba katika ujumbe ambao wakimbiza Mwenge hutoa mara nyingine wanakiuka na kujiingiza katika masuala yasiyohusu ujumbe wanaopaswa kutoa katika mbio hizo. Je, serikali inasemaje kuhusu suala hili? Maana imefikia kiasi kwamba manung'uniko haya yamejikita zaidi kwenye masuala ya siasa badala ya kupeleka ujumbe unaotakiwa!" (Bunge, 2010).

*Waziri alijibu;* "Ujumbe ambao hutolewa na wakimbiza mwenge ni ujumbe ambao dhana yake imeandaliwa na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Kwahiyo, kunakuwa na vipengele ambavyo vimeainishwa kwa mfano UKIMWI, rushwa na kadhalika. Sasa kutoka nje ya hapo, sisi hatujapata malalamiko rasmi. Kama wapo waliothibitisha hivyo hata wakati mbio za mwenge zinaendelea, tafadhali tufahamishwe mapema ili tuweze kuchukua hatua mwafaka ikiwezekana hata kumsimamisha anayefanya shughuli hizo nje ya utaratibu ambao Mwenge unapaswa kuhudumiwa."

*Swali jingine la nyongeza toka kwa Mhe. Hafidh Ali Tahir (Mbunge);* "Katika maelekezo aliyoyatoa alisema kwamba mwenge shughuli zake hasa ni kuhamasisha maendeleo, lakini vilevile kuzuia mambo ya UKIMWI na mambo mengine. Lakini Mwenge ni wa Watanzania. Mhe. Waziri anaweza kutuambia kwamba katika kumbukumbu zake za ukimbizaji mwenge, wenzetu upande wa The Civic United Front (CUF) waliwahi kukimbiza mwenge hata mara moja?"

*Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana alijibu;* "kama tulivyosema mwenge huu ni wa serikali na hauna itikadi yoyote. Wanaokimbiza mwenge chujio lao ni kamati ya ulinzi na usalama, basi. Wakishakuwa na uhakika huyu ni kijana mwenye tabia njema, sio mtu ambaye anaweza akaamua siku moja akatupa na mwenge wenyewe aone atakachofanywa; sisi tunasema tunaletewa, tunateua. Hili la kuendesha mambo bila kuzingatia itikadi yako katika maeneo mengi, kwa mfano unaweza ikawa hata 'Referee' hupaswi kuonyesha itikadi yako kama wewe ni Simba au Yanga. Unapokuwa uwanjani kazi yako pale ni kutenda haki lakini wapo 'Ma-referee' tunawafahamu hawatendi haki" (Bunge, 2010).

# VYAMA VYA SIASA

Chama cha Siasa ni maungano ya watu wanaotafuta mamlaka katika dola na hasa serikali kwa kusudi la kutekeleza shabaha za kisiasa au za kifalsafa pamoja na faida kwa ajili ya vikundi fulani au faida zao za binafsi (Wikipedia).

Tanzania ni nchi yenye mfumo wa vyama vingi vya siasa uliorejeshwa katika katiba ya Tanzania mwaka 1992. Mfumo wa vyama vingi ni hali ya kuwa na chama zaidi ya kimoja cha siasa katika nchi moja. Madhumuni ya kuwa na vyama vingi vya siasa ni kuleta ushindani wa kisiasa sio uadui kama watu wengi kwenye nchi zinazoendelea wanavyodhani. Kuwa na vyama vingi ni kuongeza wigo wa demokrasia katika jamii husika.

Vyama hutamka mwelekeo au itikadi fulani inayoandikwa katika programu yao (katiba). Katika mfumo wa vyama vingi; kipindi cha uchaguzi, vyama vinashiriki kwa kusimamisha wagombea katika nafasi ya Urais, Ubunge na Udiwani. Kila chama kinapaswa kujieleza, kutetea matendo yake ya nyuma na kuonesha jinsi kinavyotaka kuboresha mambo tofauti na vyama vingine (kampeni).

Baadhi ya vyama vya siasa nchi Tanzania ni; Chama cha Mapinduzi (CCM), Civic united front (CUF), Tanzania Labour party (TLP), Chama cha Demokrasia na maendeleo (CHADEMA), National convention for constitution and Reconstruction - Mageuzi (NCCR-Mageuzi), Alliance for change and Transparency (ACT-

Wazalendo), Chama cha ukombozi wa umma (CHAUMA), National league of Democracy (NLD)

**Itikadi (Ideology)**

Itikadi ni mkusanyiko wa imani unaoshirikiwa na kikundi cha watu fulani.

**Kuna aina kuu mbili za itikadi**

1. Itikadi za kisiasa: Ni upangiliaji unaohusu mawazo ya kimaadili na vipi nchi itaendeshwa.
2. Itikadi za Kiepistemologia: Ni upangiliaji unaohusu mawazo ya kifalsafa, ulimwengu na jinsi gani watu wanapaswa kufanya maamuzi.

Aina nyingine za itikadi ambazo zipo kwenye mlengo wa kiuchumi ni Ukomonisti, Usoshalisti na Ubepari.

**Falsafa**; ni jaribio la kuelewa na kueleza ulimwengu kwa kutumia akili inayofuata njia ya mantiki. Falsafa na itikadi za mataifa mbalimbali Barani Afrika zinatokana na matokeo ya vita kuu ya pili ya dunia.

**Itikadi kali;** ni dai la kushikilia sana misimamo ya siasa fulani au mwenendo fulani kwa kuchukua hasa maneno yaliyoandikwa na mwanzilishi bila ufafanuzi wowote, kadri unavyohitajika kutokana na muda kupita au mabadiliko mbalimbali kutokea.

(Murithi, 2018), katika Jarida lake la, "Uhusiano wa Itikadi na Mtazamo wa Mtunzi" ameeleza mitazamo mbalimbali kuhusu dhana ya itikadi. Imeelezwa; dhana ya itikadi inategemea na sababu ya sifa yake ya kuweza kutafsiriwa

kwa njia mbalimbali kutegemea malengo na dhamira ya yule anayeitumia” (Chuachua, 2011).

Sambamba na hilo (Murithi 2018), amefafanua itikadi kwa kuzingatia mikabala mitatu kama ifuatavyo;

1. *Karl Marx (1973)*

Mkabala huu unachukulia itikadi kama ung'amuzi potoshi. Katika kitabu chake cha "The Germany Ideology" Marx (1977) anasema; itikadi ni fikra zote ambazo msingi wake ni mfumo wa uzalishaji mali na teknolojia. Hujumuisha maoni ya binadamu kuhusu anavyoyasema na anayoyafikiria katika siasa, sheria, maadili, dini na falsafa. Mawazo hayo hugeuka pindi mfumo huu unavyobadilika, hivyo itikadi na jamii huendelea kubadilika. Eagleton (1976), katika 'Marxism and Literary Criticism, and criticism and Ideology'; anaonesha kuwa itikadi ni fikra, amali na hisia ambazo mwanadamu hupitia katika jamii yake kwa kipindi maalum na huweza kupatikana tu kupitia fasihi. Kuelewa itikadi ni kuelewa historia ya yaliyopita na yale ya sasa kwa undani zaidi ambayo husababisha kuzinduka na kujikomboa (Murithi, 2018).

2. Louis Althusser, (1981)

Mkabala huu unachukulia itikadi kuwa jumla ya dhana za kitamaduni ambazo hutawaliwa kupitia vyombo vya serikali na vya kiitikadi. Katika "Ideology and ideological Apparatuses" anaeleza dhana ya itikadi na kusema kuwa;

ili kuendeleza utawala na udhibiti, serikali au watawala hutumia vyombo viwili muhimu.

i. Vyombo ambavyo huendeleza utawala na udhibiti moja kwa moja kama vile wakuu wa serikali, jeshi, polisi, magereza na mahakama. Vyombo hivi hutekeleza majukumu yao moja kwa moja hivyo kwamba matakwa ya tabaka tawala hulindwa na kuhifadhiwa na kwahiyo itikadi sio ung'amuzi potoshi bali huendelezwa kwa matumizi ya nguvu.

ii. Vyombo vya kiitikadi kama kanisa, shule, vyombo vya habari, siasa, familia, sheria, vyama vya wafanyakazi, utamaduni pia hutumika kuendeleza itikadi ya tabaka tawala. Vyombo vya kiitikadi kama vile siasa hutumiwa kuhifadhi hadhi ya tabaka tawala.

Louis, (1981) anasema kuwa; Dini ilitumika zaidi kabla ya mfumo wa Kibepari kuendeleza itikadi na mawazo ya tabaka tawala. Elimu ni chombo ambacho hutumiwa na mfumo wa kibepari ambapo kila mtu huwa na itikadi inayomuandaa kwa majukumu atakayotekeleza katika jamii yenye utabaka kama wanaonyanyaswa, mshirika wa unyanyasaji, mwendelezaji wa itikadi za tabaka tawala kitaaluma na kadhalika. Watawala huweza kudhibiti watawaliwa kwa nguvu au kwa ukubalifu wao na kwa hivyo itikadi huendelezwa ambapo kila mtu huwa ameandaliwa kwa wajibu wake katika jamii ya kitabaka hasa kupitia shule (Murithi, 2018).

*3. Antonio Gramsci (1985)*

Mkabala huu unaeleza itikadi kuwa ni mfumo wa mawazo ya tabaka tawala ambalo huendelezwa kwa ukubalifu na ukawaida. Gramsci, (1985) anafafanua dhana ya itikadi kuwa ni kuendeleza dhana ya ukubalifu na ukawaida. Anasema; itikadi hupata nguvu zake kutokana na dhana ya ukubalifu kinyume na matumizi ya nguvu. Jamii huendelea kuwa na umoja na udhibiti huendelezwa kwa nguvu za mamlaka kama vile polisi na jeshi au kwa vigeu vingine kama jinsia, rangi, kabila na utamaduni. Hali hizi huchukuliwa kwamba ni zakawaida au za kimaumbile na kwahiyo wanaonyanyaswa huenda hata wasijue wananyanyaswa (Murithi, 2018).

# BAJETI YA MBIO ZA MWENGE

Bajeti kubwa ya mbio za mwenge inayopelekea wananchi kuchangishwa michango ya lazima. Baadhi ya watu hubeza mbio za mwenge wa uhuru na kupunguza mahaba. Sababu nyingine kubwa ni bajeti ya mwenge kila mwaka na michango inayochangishwa kwa wananchi kufanikisha shughuli hiyo.

## Nini maana ya mchango?

Kamusi ya Kiswahili sanifu inaeleza maana ya mchango ni; mali na fedha sinazokusanywa kwa ajili ya kutekeleza jambo fulani.

Wanajamii wanautamaduni wa kuchangiana kwenye shughuli za furaha au huzuni mfano ndoa, shughuli za mazishi, sherehe mbalimbali za kijamii, na maadhimisho au matamasha. Utamaduni huo unawafanya washiriki wote kuichukulia shughuli husika kuwa ni ya kwao na sio ya mtu mmoja au kikundi cha watu waliyoianzisha au kuandaa. Hivyo washiriki (wachangaji) nao wanapata uwezo unaopelekea kumwajibisha mwenye shughuli, iwapo atakwenda kinyume na makubaliano. Ili kufanikisha hilo, shughuli nyingi washiriki wanaunda kamati mbalimbali za utekelezaji na usimamizi.

Majibu ya bajeti ya mbio za mwenge wa uhuru na michango yake pamoja na hali halisi ya mtazamo wa wananchi kuhusu jambo hilo linajieleza kutokana na

 © 2020

mijadala na matamko ya viongozi mbalimbali wa nchi kama ifuatavyo;

*Mei 27, 2014 Bungeni Dodoma; Mhe. Lucy Owenya (Mbunge viti maalum) aliuliza swali;* "Kiasi gani cha fedha hutumika kwa kila wilaya kwa ajili ya mbio za mwenge, gharama za kuuwasha na kuuzima na faida gani zinazopatikana?" (Bunge, 2014).

*Swali hilo lilijibiwa na Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Mhe. Juma Nkamia. Alisema*; "Serikali hutenga fedha kulingana na mahitaji ya gharama halisi ya wakati husika. Mfano, mwaka 2012 Tsh. Milioni 650 zilitengwa kwa ajili ya kuadhimisha uzinduzi na kilele cha mbio za Mwenge wa Uhuru ambazo kati ya hizo Sh. Milioni 450 zilitumika na Wizara na Sh. Milioni 200 zilitumika na mkoa mwenyeji wa kilele cha mbio hizo" (Bunge, 2014).

***Faida***

*Alisema;* "Mbio za Mwenge zinaeneza ujumbe wenye manufaa kwa jamii. Pia ni kuendelea kutunza historia na falsafa ya ukombozi wa Taifa, kuhamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa kuendelea kuenzi amani, mshikamano, upendo na zaidi kupambana na aina yoyote ile ya kuwabagua Watanzania kwa rangi, dini au makabila yao. Kuendelea kuhamasisha wananchi kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali na kujiletea maendeleo" (Bunge, 2014).

*Swali la nyongeza liliulizwa na Mbunge wa jimbo la Ubungo Mhe. John Mnyika na alitaka kujua hatua zinazochukuliwa ikiwa*; mwenge unaongeza ugumu wa maisha kwa kuchangisha wananchi michango na kuwa viongozi wa mbio hizo mwaka huu (2014) wanapita kupiga propaganda ya serikali mbili. Mwishoni mwa swali, Mbunge alitaka mbio za mwenge zifutwe, (Habari leo, 2014).

*Mhe. Juma Nkamia, Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo alijibu*; "Serikali haiko tayari kusitisha mbio hizo, kwani wananchi wanaimani nazo na zimesaidia kudumisha umoja na amani," (Bunge, 2014).
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu; Sera, Uratibu na Bunge Mhe. William Lukuvi alisema*; "Michango hiyo ni hiari na hakuna anayelazimishwa kuchangia, na kwamba hailipii mafuta ya mwenge wala posho za wakimbizaji," (Bunge, 2014).

Mhe. Mizengo Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Alisisitiza na kusema; "Nimesimama kwasababu nimesikiliza mjadala hapa naona jambo hili kubwa, linaonekana kama halina maana kwa Taifa. Kila mwaka, mbio za mwenge huwa na kauli-mbiu mahsusi kwa sababu mwenge huu huwa na fursa ya kufika maeneo mengi hivyo kufikisha ujumbe kuhusu masuala mazito ya nchi kama elimu. Kwa hiyo si sahihi kabisa kuona Mwenge wa uhuru hauna maana. Hili linaweza lisiwapendeze sana wenzetu wa upande wa pili.

Mwenge unahimiza suala la kujitolea katika shughuli zao za maendeleo. Wananchi wanahimizwa kuenzi moyo huo na wamekuwa wakifanya hivyo katika shughuli mbalimbali za kijamii. Hili halina ukakasi hata kidogo; hoja hapa imekuwa ni michango, lakini hivi mwenge unakuja pale kwangu kibaoni, kwa ugeni huo unaofanyakazi nzuri; kama watu wanachanga kuku, bata, hii sio dhambi. Wananchi wamekuwa wakarimu sana katika jambo hili" (Bunge, 2014).

Baada ya Mhe. Mizengo P. Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoa ufafanuzi, wabunge wa upinzani walisimama na kuomba mwongozo kuhusu majibu hayo ya mawaziri. Hoja yao ilikuwa; wananchi wanachangishwa michango ya kugharamia mbio za mwenge. Baadhi yao walisoma jumbe walizotumiwa na wananchi katika simu zao za mkononi. Waliosimama ni; Mhe. Susan Kiwanga - Viti maalum (Chadema), Mhe. Ezekiah Wenje, Mbunge wa Nyamagana (Chadema), na Mhe. Moses Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini.

*Ulazima wa kuchangia Mwenge wa Uhuru haukuwa wa nchi mzima sawa na viongozi walivyoeleza bali kwa sababu mbalimbali baadhi ya halmashauri walikubaliana kuchangishana. Kitendo cha kuchapisha barua au matangazo ya michango kwa njia ya mtandao kumesababisha hata wasiochangishwa wapaze sauti kuwa wanasumbuliwa. Mfano wa machapisho mtandaoni yanayoweza kusababisha taharuki kwa wananchi juu ya*

*michango ya Mwenge wa uhuru ingawa michango hiyo huchangwa kwa hiari.*

Naibu Spika Mhe. Job Ndugai alisema atatoa majibu ya mwongozo huo "Mbele ya safari." Kabla ya mjadala huo kuibuka bungeni, Waziri Mkuu Mhe. Mizengo Pinda alishawahi kueleza umuhimu na faida za mwenge wa uhuru katika hotuba zake. Moja ya hotuba hizo ni ile ya tarehe 29 Mei 2008 katika kijiji cha Msoga wilayani Bagamoyo, kwenye sherehe ya uzinduzi wa mbio za mwenge wa uhuru. *Alisema*;

"Mbio za mwenge wa uhuru ni tukio la kihistoria. Eneo ambalo mbio za mwenge wa uhuru zinazinduliwa kwa kawaida ni mahali penye jambo fulani la kihistoria. Mwenge wa uhuru unapowashwa hukumbusha wananchi historia hiyo au huanzisha historia mpya katika eneo hilo. Hivyo, ni dhahiri hapa katika kijiji cha Msoga lipo jambo kubwa la kihistoria. Napenda kuwafahamisha Watanzania wenzangu na wananchi wote kuwa hapa tulipo leo hii ndipo mahali ambapo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, alipozaliwa na kukulia (Habari leo, 2014).

"Uzoefu unatuonesha kuwa umuhimu wa mbio za mwenge wa uhuru unazidi kuongezeka mwaka hadi mwaka. Kama nilivyowahi kusema tunauhitaji *mwenge wa uhuru kama ishara ya kuleta matumaini, upendo, heshima na maendeleo kwa Watanzania*. Mwenge wa uhuru ni kichocheo cha kuleta maendeleo ya wananchi na taifa letu kwa haraka.

"Aidha, dhana ya mbio za mwenge inaendelea kupata umaarufu duniani kote. Hivi karibuni tulishuhudia ujio wa Mwenge wa Olimpiki ambao umekimbizwa katika miji kadhaa duniani. Lengo lake ni kuleta amani, upendo na matumaini. Mbio za mwenge wa uhuru zinatukumbusha maneno ya busara na hekima yaliyotamkwa na Baba wa taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere." ......Katika kuenzi fikra na hekima za marehemu Baba wa taifa Mwalimu J. K Nyerere, kila Mtanzania anao wajibu wa kuhakikisha kwamba anadumisha amani, upendo, matumaini na kuepuka aina ya maneno na matendo yanayoweza kuleta chuki miongoni mwetu. Nchi yetu bado inaendelea kuwa na amani na ushirikiano licha ya kuwa moja ya nchi kubwa Afrika yenye makabila zaidi ya 120, dini tofauti na itikadi tofauti. Aidha, wananchi wanaendelea kuheshimiana, kupendana na kutofautiana kifikra bila kupigana. Tumefanikiwa kujenga U-TANZANIA. Naamini kwamba, pamoja na mambo mengine, mbio za Mwenge wa Uhuru zimechangia katika kudumisha amani, upendo na mshikamano" (Habari leo, 2014).

*Ingawa kumekuwa na maelezo mazuri ya viongozi kipitia vyombo mbalimbali na kueleza kuwa michango ya mbio za Mwenge wa uhuru ni hiari, lakini kwa upande wa wananchi bado malalamiko ni mengi kuhusu kuchangishwa michango ya lazima. Tatizo ni nini?*

Baadhi ya Halmashauri za Wilaya na Miji kutotii maagizo na kuendelea kuchapisha matangazo ya michango, kwa uchache wao lakini iliweza kuleta taharuki kwa wananchi

na kuhisi serikali inawachangisha michango ya mbio za Mwenge kwa lazima. Hali hii inachangia baadhi ya wananchi kuuchukia mwenge wa uhuru kwa kuwa matangazo ya umuhimu wake ni machache kuliko mabango ya michango. Kwa mfano mwezi Mei, 2013; kwenye mitandao ya kijamii ilichapishwa habari inayohusu walimu wote wa Shule za Msingi wilaya ya Manyoni, kuwa Afisa Elimu msingi (W) Bi. Julieth Binyura amewachangisha Tsh. 3000 kwa kila Mwalimu kwa ajili ya shughuli za mwenge wa uhuru. Pia baada ya mijadala ya bungeni kuhusu michango hii, mwezi Agosti, 2014; Mkuu wa wilaya ya Sengerema alitoa agizo kwa watumishi wote wa kata za Halmashauri ya wilaya Sengerema idara ya Afya, Elimu na kilimo kutoa mchango wa Tsh 1000 kwa ajili ya mafuta ya mwenge na Tsh. 10,000 kwa ajili ya ujenzi wa maabara za shule katika kata husika. Agizo hilo liliwataka Watendaji wa kata kukusanya fedha hizo kwa kuorodhesha majina ya watumishi wote watakaochanga na wasiochanga kiwango hicho.

"Wawekezaji na wafanyabiashara wakubwa na wadogo Wilayani Muheza Mkoani Tanga ambao watagoma kuchangia fedha za maandalizi ya ujio wa mwenge wa uhuru katika wilaya hii, wafungashe vilago kwani watakuwa hawatufai." Kauli hiyo ilitamkwa April 2016 na Mkuu wa Wilaya ya Muheza Bi. Esterina Kilasi katika kikao cha maandalizi ya ujio wa mwenge wa uhuru, (Nipashe, 2016).

Mei 22, 2017 gazeti la Mwananchi liliandika habari kuhusu Mbunge wa viti maalum Mhe. Rhoda Kunchela alilipotiwa akisema; "Mkononi hapa nina risiti zaidi ya 300 za michango iliyochangishwa kwa baadhi ya watendaji wa serikali wakiwepo walimu, wafanyabiashara na wafanyakazi wa kada mbalimbali. Ni malalamiko ya muda mrefu sana kwamba wamekuwa wakilazimishwa michango hii. Kibaya zaidi serikali iliwahi kutoa taarifa hapa bungeni kuwa michango hii ni hiyari. Tulipofikia sasa hivi si sawa kwa mikoa mbalimbali kuendelea kulazimishwa kuchangia mwenge wa uhuru wakati ni hiari. Jambo hili serikali itoe tamko au Bunge lako lijadili suala hili" (Mwananchi, 2017).

Mwenyekiti wa bunge, Mhe. Andrew Chenge alikataa kuruhusu hoja hiyo ijadiliwe na kumtaka Mbunge kukabidhi risiti hizo kwa Bunge ili wazikabidhi serikalini kwa hatua zaidi (MwanaHALISI, 2017).

Hadi kufikia Mwaka 2018, katika Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo - Tukuyu Mkoani Mbeya; Daniel Mwamasangula Kaimu Afisa Elimu (W) Msingi, kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (DED) aliwaandikia barua walimu wakuu wa Shule za Msingi zilizopo katika Halmashauri hiyo yenye kumb. Na BDC/J.I/04/137 ya tarehe 23 Januari 2018 na kichwa cha Habari "MCHANGO WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2018".

Barua hii, Afisa Elimu aliwataka walimu kuonesha ushirikiano kwa kuchangia kiasi cha Tsh. 10,000 kila shule (mchango wa shule), Mkuu wa shule Tsh. 20,000 na

walimu wengine Tsh. 5000. Akaunti iliyokusanya michango ni 61410001908 Miscellaneous Deposit Busokelo. Mwisho wa kuchangia ilitajwa ni tarehe 17 April, 2018; Wakuu wa Shule wawasilishe idadi ya walimu waliochangia na wasiochanga kwa majina (JamiiForums, 2018).

Huko Karagwe kupitia tovuti ya halmashauri; Afisa habari wa Halmashauri, Innocent Mwalo alichapisha tangazo linalowahusu watumishi wote na umma kwa ujumla. Tangazo lilielekeza yafuatayo;

“Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya Karagwe, Godwin M. Kitonka anapenda kuwaomba watumishi na wananchi wote wa halmashauri ya wilaya kwa ujumla kuchangia mbio za Mwenge wa Uhuru unaotarajiwa kuzindua miradi mbalimbali ya maendeleo wilayani hapa mnamo Agosti 04, 2017.

‘Ikiwa ni azimio lililofikiwa kwenye kikao cha kamati ya Mwenge wa Uhuru kilichoketi mapema mwishoni mwa mwezi April mwaka huu, kila Mkuu wa idara katika halmashauri hii anaombwa kuchangia kiasi cha Tsh. 30000/= huku maafisa wengine wakiombwa kuchangia kiasi cha Tsh. 10,000/= kila mmoja.
Wakuu wa shule za msingi na sekondari pamoja na Waratibu kata watapaswa kuchangia kiasi cha Tsh. 20,000/= kila mmoja.

‘Aidha, walimu wa shule za sekondari, wahudumu na madereva wanaombwa kuchangia kiasi cha Tsh.5000/=

‘kila mmoja huku walimu wa shule za msingi wakitakiwa kuchangia kiasi cha Tsh. 3,000/= kila mmoja. Hata hivyo, Afisa biashara wilaya anaagizwa kukusanya michango kwa baadhi ya vyombo vya moto ambapo kila teksi inaombwa kulipa kiasi cha Tsh. 5000/= na kwa upande wa mabasi kila moja likitakiwa kuchangishwa kiasi cha Tsh. 50,000/= kwa upande wao wafanyabiashara wadogo wanaombwa kuchangia kiasi cha Tsh. 10,000/= kila mmoja.

‘Shule na Taasisi binafsi na wazabuni wote wanaombwa mchango wa kiasi cha Tsh. 50,000/= kila mmoja, huku shule za msingi na sekondari za serikali zikiombwa kiasi cha Tsh. 20,000/=

Ikumbukwe kuwa kila Mkuu wa idara na yeyote aliyepewa jukumu hilo la ukusanyaji atapaswa kutoa taarifa ya ukusanyaji katika kila kikao cha kamati ya mwenge kitaifa kitakapokaa. Inashauriwa kuwaelimisha wachangiaji kuona umuhimu wa kuchangia mchango huu kwani mchango huu ni wa hiari” (Karagwe, 2017).

*Watu walihoji kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri kwa mujibu wa sheria za nchi, yeye ndiye Mwajiri wa watumishi wote katika halmashauri husika. Kwa maelekezo aliyoyatoa kwa watumishi wake, kuna fursa ya hiari katika utekelezaji*?

Mwishowe mwarobaini wa mijadala yote ya hoja za michango ya mwenge wa uhuru ukapatikana, baada Viongozi wa mbio za mwenge kupewa jukumu la kufuatilia

na uhalali wa michango hiyo kama ilivyofafanuliwa kwenye hotuba ya Mhe. Kasimu Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye uzinduzi wa mbio za mwenge wa uhuru Mkoani Geita tarehe 2 Aprili, 2018.

Waziri Mkuu *alisema*; "Falsafa hii ya mwenge wa uhuru siyo tu inatukumbusha historia na harakati za kadai uhuru, bali ndiyo msingi wa sera zetu za ndani na nje ya taifa letu. Mifano ya matokeo chanya ya falsafa hii tangu mwenge wa uhuru ulipowashwa hadi sasa ni pamoja na, mapinduzi matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964 yaliyoondoa utawala wa Kisultani, Muungano wa Tanzania, Azimio la Arusha la mwaka 1967 lililosisitiza Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, sera madhubuti ya nje ya kutofungamana na siasa za upande wowote, ushiriki wa Tanzania katika ukombozi wa nchi za Kusini mwa Bara la Afrika ambapo Tanzania ilikuwa makao makuu ya kamati ya ukombozi Kusini mwa Afrika na kichocheo kikubwa katika kuhamasisha wananchi kujiletea maendeleo yao wenyewe. Falsafa hiyo ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ilikuwa ni ujumbe mzito kwa Waingereza kwamba, watu wa Tanganyika wamechoka kutawaliwa" (PMO, 2018).

" ......Hivyo, kama Mhe. Rais wetu mpendwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alivyosema mnamo tarehe 14 Oktoba, 2017 huko Zanzibar wakati wakuhitimisha mbio za mwenge wa uhuru mwaka jana; busara na hekima zilizojengwa chini ya falsafa ya mwenge wa uhuru,

hazitaachwa na kupotea. Serikali itaendelea kuienzi falsafa hii kwa vitendo na kuifanya kuwa endelevu kwa vizazi vijavyo na kwa maslahi mapana ya Watanzania, Afrika na dunia kwa ujumla." *Alihitimisha hotuba yake kwa kusema*; "Naomba sote tushirikiane kumuomba Mwenyezi Mungu awajalie afya njema na safari ya salama vijana tutakaowakabidhi jukumu la kukimbiza mwenge wa uhuru kitaifa kwa siku 195 nchi mzima ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Napenda kuwakumbusha kuwa;

i. Mnatakiwa kutekeleza jukumu hili kubwa na nyeti kitaifa kwa bidii, juhudi, nidhamu, uadilifu na weledi wa hali ya juu.

ii. Kukagua na kufuatilia miradi ya maendeleo kwa kulinganisha thamani ya fedha na hali halisi ya miradi ilivyo.

iii. Kuchunguza kwa umakini jinsi michango ya mwenge ilivyotolewa na matumizi yake.

iv. Mwisho, kutoa taarifa ya matokeo ya kazi yenu serikalini bila woga wala shinikizo la mtu yeyote na sisi tutaifanyia kazi," (PMO, 2018).

***

## HISTORIA YA UKOMBOZI WA TANGANYIKA

Tujikumbushe waliyopitia Watanganyika kabla ya uhuru, mambo ambayo yalipelekea Mwalimu Julius Kambarage Nyerere pamoja na Wanachama wenzake wa chama cha TANU kuuwasha mwenge wa uhuru na kuuweka juu ya kilele cha mlima Kilimanjaro.

Baada ya Vita Kuu ya pili ya Dunia mwaka 1945, utawala wa Waingereza uliimarisha mipango ya kilimo kwa Waafrika na kuchochea upinzani dhidi ya ukoloni katika sehemu kubwa ya nchi. Sera za kikoloni zilileta mabadiliko ya kiuchumi na kijamii ambayo yaliongeza tofauti za kijimbo na ushindani kati ya makundi ya waliopata elimu katika kuendeleza sehemu walikokuwa wakitoka. Matokeo yake yakawa ni kuanzishwa kwa vyama vya kikabila ambavyo vilitumiwa kuelezea upinzani dhidi ya sera zilizokuwa hazifai yaani ukoloni (Wikipedia).

Baadhi ya sehemu utaratibu huo ulileta mafanikio makubwa ya kudai kuwa na Machifu wa kuimarisha umoja wa kikabila. Chama cha Tanganyika African Association (TAA) ambacho kilianzishwa mwaka 1922 kama chama cha ustawi wa watumishi wa serikali. Hadi kufikia miaka ya 1930 chama hicho kilikua na kuanzisha matawi katika majimbo ambayo yalisaidia sana katika kuimarisha nguvu ya makao makuu ya chama hicho (Juzuu, 1999).

Baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia, upinzani ulijitokeza nchini kote ukiwa umejikita katika nyanja za kijamii ulielekea kukidhoofisha chama hicho. Lakini upinzani dhidi

ya sera za kikoloni ndiyo ulitokea kuwa moja wapo ya mihimili muhimu katika chama cha kizalendo. Kichocheo cha nguvu yake kilitoka Jimbo la Ziwa, eneo la Tanganyika ambalo lilizalisha karibu nusu ya thamani ya bidhaa zote za kilimo zilisafirishwa nje.

Upinzani dhidi ya ukoloni uliwekwa kuhusu mazao ya kilimo yaliyotokea katika jimbo lote na tawi la TAA, chama kiliingilia kati na kuwaunga mkono wananchi katika malalamiko yao. Hivyo ikawa inaunganisha chama cha ustawi wa wafanyakazi mjini na kuzungumzia matatizo ya vijijini.

Mwaka 1952 nguvu ya chama ilififia sababu viongozi wa wafanyakazi na wasomi wa mjini waliokuwa wanaongoza kupigwa vita na wasemaji hodari walihamishwa Dar-es-salaam. Hivyo kukawa hakuna mikutano, lakini kiongozi mpya akatokea na kuratibu shughuli za chama. Kiongozi huyo alikuwa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Mnamo tarehe 7 Julai, 1954 yaani baada ya miaka miwili (2) chama cha TAA kikawa kimebadilika na kuwa chama kamili cha siasa ambacho kilipewa jina la Tanganyika African National Union (TANU), (Juzuu, 1999).

Mwaka 1961, chama cha TANU kikaleta uhuru wa taifa la Tanganyika. Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliweza kuitumia vizuri nafasi ya kimataifa ya Tanganyika kama nchi ya udhamini chini ya umoja wa Mataifa ili kuhakikisha kuundoa ukoloni.

## Historia ya vyama vingi vya siasa na usaliti kabla ya uhuru

Mwaka 1946, Tanganyika chini ya 'League of Nations' mamlaka yalibadilishwa na kuwa nchi ya udhamini. 1956, Edward Twining akiwa Gavana wa Tanganyika (Muingereza) akawashawishi wajumbe wengi wasio-rasmi wa baraza la kutunga sheria ambao walikuwa wameteuliwa badala ya kuchaguliwa ili waunde chama cha upinzani ambacho kilijulikana kama United Tanganyika Party (UTP) ili kipingane na chama cha TANU. Chama hicho yaani UTP baadae kilianza kufifia na hadi kufikia 1960 chama cha TANU kikashinda viti 70 kati ya 71 katika uchaguzi wa kwanza wa kugombea viti vya Baraza la kutunga sheria. Kwa kufuata utaratibu wa kura, iliwezekana sasa Waafrika kushinda uchaguzi. Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akawa Waziri Kiongozi wa Serikali ya Tanganyika ambayo kwa muda huo ilikuwa haiongozwi tena na Waingereza. Ilipofika tarehe 9 Desemba 1961, Tanganyika ikawa nchi ya kwanza katika Afrika Mashariki iliyokuwa inatawaliwa na Uingereza, kupata Uhuru kamili (Wikipedia).

***Ukombozi wa fikra***; Siasa za vyama vingi Barani Afrika zina hisia za kukosa uzalendo. Kama kuna Waafrika walirubuniwa kuwasaliti Waafrika wenzao kwa kuunda vyama vya siasa vyenye sera za ukombozi wa wananchi wakati nyuma ya pazia wanalengo la kuvunja umoja uliojengwa na waungwana ili kujipatia uhuru na haki ya kweli. Matokeo yake walichelewesha kumwondoa mkoloni

katika nchi zao. Vimelea hivi vya usaliti vinaweza kuendelea kuwepo miongoni mwa wananchi. Hivyo si vibaya wananchi wakafuata sera za vyama vya siasa badala ya kushabikia watu au vikundi vya watu wanaochochea machafuko kwa mgongo wa demokrasia.

## Kwanini nchi ya Tanganyika ilikuwa na hadhi ya Nchi ya Udhamini?

Uhuru umetokea mbali, wahenga husema kila pafukapo moshi kuna moto. Tuamini mwenge wa uhuru uliwashwa kwa imani na matumaini makubwa.

Tanganyika ilikuwa chini ya mikataba ya kibepari kama ilivyoelezwa kwenye (Juzuu, 1999), Historia Kuu ya Afrika kama ifuatavyo;

### Historia

Mkataba wa Versailles wa mwaka 1919 wenye kanuni za kuchukua makoloni yote ya Ujerumani na kukabidhi kwa mataifa washindi wa vita ya Kwanza ya Dunia. Hivyo Tanganyika ilikabidhiwa rasmi mikononi mwa miliki ya Uingereza kama eneo la kudhaminiwa chini ya mamlaka ya Shirikisho la Mataifa 'League of Nations'. Kifungu namba 22 cha katiba ya Shirikisho la Mataifa lilieleza;

"Makoloni na maeneo ambayo kutokana na matokeo ya vita iliyopita si tena chini ya mataifa yaliyowahi kuyatawala. Yakikaliwa na mataifa ambayo hayapo tayari kujisimamia katika mazingira magumu ya dunia ya kisasa

(kujitawala). Hivyo mataifa hayo yatatazamiwa kwa udhamini wa ustaarabu wa kimataifa. Njia bora yakutekeleza nia hii itakuwa kukabidhi malezi ya mataifa hayo mikononi mwa mataifa yaliyoendelea ambayo yapo tayari kukubali ulezi huu. Nawakabidhi kwa niaba ya Shirikisho la Mataifa," (Juzuu, 1999).

*Katiba ya Shirikisho la Mataifa ilitofautisha maeneo ya udhamini kama ifuatavyo:*

a) Jumuiya zilizokuwa chini ya miliki ya Uturuki; zilikuwa kwenye ngazi ya kukubaliwa kama mataifa ya pekee lakini bado chini ya usimamizi wa nchi mlezi hadi wakati zitakapoweza kusimama pekee yao. "Jumuiya hizi zinapaswa kusikilizwa kuhusu chaguo la nchi mlezi."
b) "Mataifa yale yako katika hali ya kwamba mlezi atawajibika kutawala maeneo yao kwa masharti ya kuhakikisha uhuru wa dhamiri na wa dini, kutunza usalama na maadili mema na kuzuia dhuluma kama biashara ya watumwa, silaha na vileo mfano Afrika ya kati.
c) "Maeneo kama Afrika ya Kusini-Magharibi na visiwa kadhaa vya Pasifiki ya Kusini. Ambayo yatasimamiwa na mlezi kulingana na sheria zake kama sehemu ya eneo lake kwa sababu yanawakazi wachache mno au ni madogo mno au yako mbali mno na vitovu vya ustaarabu. Hata hivyo utawala huo unapaswa kuangalia masharti

yaliyotajwa kuhusu masharti yanayotunza wakati wazalendo."

**Maeneo ya kudhaminiwa ya kundi yalitengwa katika makundi A, B, na C**

*A. Maeneo yalikuwa sehemu za miliki ya Osman (Waturuki) chini ya ulezi wa Uingereza; (Uhuru kati ya 1932 - 1946)*

| | |
|---|---|
| Palestina | 1946 |
| Yordani | 1946 |
| Iraq (Mesopotamia) | 1932 |

**Chini ya Ufaransa**

| | |
|---|---|
| Syria | 1946 |
| Lebanon | 1943 |

*Maeneo yakudhaminiwa ya kundi B; nchi hizi zilikuwa zote koloni za Ujerumani katika Afrika*

i. Chini ya ulezi wa Ufaransa hadi uhuru mwaka 1960 ni, Cameroon na Togo.
ii. Chini ya ulezi wa Uingereza; Tanganyika 1961, sehemu ndogo ya Cameroon na Togo.
iii. Chini ya ulezi wa Ubelgiji; Ruanda - Urundi na uhuru kama nchi mbili yaani Rwanda na Burundi 1962.

*Kundi C; kundi hili lilijumlisha maeneo mengine yaliyokuwa chini ya Ujerumani*


© 2020

## Maeneo yote ya kudhaminiwa

1. Syria (Ufaransa)
2. Lebanon (Ufaransa)
3. Palestina (Uingereza)
4. Ng'ambo ya Yordan (Uingereza)
5. Iraq (Uingereza)
6. Togo (Ufaransa)
7. Togo (Uingereza)
8. Cameroon (Uingereza)
9. Cameroon (Ufaransa)
10. Ruanda – Urundi (Ubelgiji)
11. Tanganyika (Uingereza)
12. Afrika ya Kusini - Magharibi (Afrika ya Kusini) - (Uingereza)

(Chanzo: Juzuu, 1999).

## Matukio muhimu yaliyotokea Tanganyika kabla ya Uhuru

Kabla ya uhuru wa Tanganyika, kulitokea matukio yawezekana ndiyo yaliyopelekea mwenge wa uhuru kuwashwa na kuwekwa juu ya kilele cha mlima Kilimanjaro ili umulike Bara zima la Afrika.

*Kutawaliwa kwa Watanganyika kulianza lini?*

Karne ya 15, Wareno walilifanya eneo la Mashariki ya Ziwa Tanganyika na Kusini mwa Afrika kuwa lao. Wareno

walizidiwa nguvu kwa eneo la Mashariki ya Ziwa baada ya ujio wa Sultani wa Oman karne ya 17 na kutawala akifanya biashara ya Watumwa. Ujerumani ilitawala Tanganyika karne ya 19, kuanzia mwaka 1886 baada ya mkutano wa Berlin, hadi 1919 baada ya Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia. Uingereza ilitawala kuanzia mwaka 1919 hadi 1961 ikiwa chini ya Udhamini wa Shirikisho la Kimataifa, (Juzuu, 1999).

## Mkutano wa Berlin

Novemba 15, 1884 hadi Februari 26, 1885 mjini Berlin Ujerumani kulifanyika Mkutano Mkuu wa Kimataifa kuhusu nchi za Ulaya katika Afrika. Mkutano huo, uliweka msingi wa ugawaji wa Bara la Afrika kati ya madola ya mataifa ya Ulaya (Wikipedia).

Kukaliwa kwa baadhi ya maeneo ya Afrika na mataifa ya kigeni tangu karne ya 17 hasa kwenye Pwani za Afrika kwa sababu za kibiashara na sio kiutawala. Mwanzoni mwa karne ya 19, biashara ziliyumba baada ya gharama za uzalishaji kuwa kubwa kuliko faida pindi miliki ya Uingereza, kutangaza kukomesha biashara ya watumwa, (Juzuu, 1999).

***

*MWENGE WA UHURU mulika na huko wasije kusema; hawakuona kwasababu walikuwa gizani.*

 © 2020

Tanzania imebahatika kupata Marais wenye maono ya kifalsafa. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan anasema; KAZI IENDELEE!”

**MWISHO**

## REJEA

Abdallah Said Hancha, (2015), SIBANDUKI AFRIKA, Hancha Books, Dodoma - Tanzania. ISBN 978 9987 9856 0

Andrew O. Urevbu B.Sc. (Ed.), M.Ed PhD, (1985), CURRICULUM STUDIES, Longman Singapore Publishers pte Ltd, Singapore. ISBN 0 582 06604 2

Bunge la Tanzania, (2014), MAJADILIANO YA BUNGE, MKUTANO WA KUMI NA TANO, KIKAO CHA KUMI NA TISA, Bunge – Dodoma, Tanzania (Mei 27, 2014)

Bunge la Tanzania, (2017), MAJADILIANO YA BUNGE, MKUTANO WA SABA, KIKAO CHA KUMI NA NANE, Bunge – Dodoma, TANZANIA (Mei 5, 2017)

George Bishop, (1985), CURRICULUM DEVELOPMENT: A Textbook for Students, Macmillan Education Ltd, London, UK. ISBN 0 – 333 – 39118 – 7

James Elisa Chalambo Jesse (2009), FREEDOM OF SPEECH FOR MEMBERS OF PARLIAMENT IN TANZANIA, University of Dar-es-Salaam, Africa publishing (T) Ltd, Dar-es-Salaam Tanzania. ISBN 9966-7237-3-0

John C. Maxwell, THE 21 IRREFUTABLE: LAWS OF LEADERSHIP Limited Edition. Manu Graphics Books, New Delhi, India. Uk na. 52

Kagasheki M. Edwin, (2016), IJUE HISTORIA YA KUANZISHWA KWA MWENGE, Parmalink

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, (2005), KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA YA MWAKA 1977, Mpiga chapa Mkuu wa serikali, Dar es Salaam – Tanzania. Uk na. 14

Lee Kuan Yew, (2000), FROM THIRD WORLD TO FIRST, THE SINGAPORE STORY: 1965-2000, Marshall Cavendish editions; 1 new industrial road – Singapore. Uk na. 169

Lee Kuan Yew (1998), THE SINGAPORE STORY: MEMOIRS OF LEE KUAN YEW, Marshal Cavendish editions, Singapore. ISBN 978-981- 4276 177

Murithi Joseph Jessee, (2018), UHUSIANO WA ITIKADI NA MTAZAMO WA MTUNZI, Journal of Humanities and social science (IOSR-JHSS). Volume 23, issue 9, ver. 4 (September. 2018) 75-83, www.iosrjournals.org

Mwalimu Julius Nyerere (The Mwalimu Nyerere Foundation), (2004), NYERERE KUHUSU ELIMU, Oxford University Press, Dar es Salaam – Tanzania. ISBN 9987 – 8943 – 5 – 6

Mwalimu Julius Nyerere (The Mwalimu Nyerere Foundation), (2006), NYERERE KUHUSU ELIMU VOLUME II, Oxford University Press, Dar es Salaam – Tanzania. ISBN 9987 – 423 – 16 – 7

Oxford, (2015), ADVANCED LEARNER'S DICTIONARY, New 9th Edition, Oxford University Press, United Kingdom.

Pius Msekwa, (2012), UONGOZI NA UTAWALA WA MWALIMU JULIUS KAMBARAGE NYERERE: Miaka 25 ya utumishi wangu kwa umma chini ya uongozi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Nyambari Nyangwine Publishers, Dar-es-salaam Tanzania.

Pius Msekwa, (2013), 50 YEARS OF INDEPENDENCE: A CONCISE POLITICAL HISTORY OF TANZANIA, Nyambari Nyangwine Publishers, Dar-es-salaam Tanzania. ISBN 978-9987-0915-22

Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili (TUKI), (1999), HISTORIA KUU YA AFRIKA, VIII AFRIKA KUANZIA 1935 (JUZUU LILILOFUPISHWA), Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam (UDSM), Dar-es-Salaam -Tanzania

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI), (2004), KAMUSI YA KISWAHILI SANIFU, toleo la pili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania

Tanzania, (1968), REVOLUTION BY EDUCATION, Longmans of Tanzania Limited, Arusha – Tanzania

Willibrod Peter Slaa, (2018), NYUMA YA PAZIA, Readit Books Ltd. Dar-es-salaam, Tanzania. ISBN 978 9987 21133 3

Wizara ya Eimu na Utamaduni, (1997), SERA YA UTAMADUNI, Tovuti ya serikali, Dar es Salaam – Tanzania

**Magazeti**

Habari leo, Mei 28, 2014, Mei 17, 2019 na Oktoba 14, 2017
MwanaHALISI, Mei 22, 2017
Mwananchi, Mei 22, 2017
Nipashe, Mei 22, 2017
Rai, Julai 25, 2019, na Desemba 15, 2016

**Mtandao na Tovuti**

Http://www.en.wikipedia.org
Http://www.tanzania.go.tz
Http://www.dw.com Juni 5, 2000, Aprili 24, 2013, na Aprili 3, 2014,
Http://www.rfi.com Julai 26, 2018
Http://www.dodomafm.com Mei 30, 2018
Http://www.mojasky.com Juni 20, 2019
Http://www.bbc.com Octoba 22, 2015, na Februari 21, 2019
Http://www.zoomtanzania.com Februari 24, 2017
Http://www.michuzi.blog Desemba 23, 2008
Http://www.pmo.go.tz (pm-speeches)
Http://www.Karagwedc.go.tz
Http://www.zanzibar24.com.tz Desemba 21, 2017